**ZITTO** ajitosa madeni ya mbolea, Katibu Mkuu Kilimo amjibu

UKURASA 5



**MAHAKAMA** Kuu yatengua uamuzi wa IGP kuwafuta kazi askari polisi

UKURASA 8



**BADO** siku mbili mbivu, mbichi watakaopata mikopo elimu

UKURASA 3


ama

AFYA NA MAZINGIRA

Vijue viru... vinavyolinda mwili w... binadamu, vinakwepa... na bakter...

...TAILI NNE ZA MIUNDOMBINU...
...simulizi ya miaka mitatu ya Awamu VI,
...livyopokea MMAM kwa mtaji majengo

KILICHOWABEBA RAIS AKAWASIFIA...

**Mapinduzi maji Tanga kutoka hatari ...ukame, hadi mwelekeo kujitosheleza**

Dk. Mpango naye, 'mfano kuigwa kujitegemea kifedha'

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Septemba 19, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581804

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Kaburi la mtoto lafukuliwa usiku

**SANDA**, jeneza, msalaba vyawekwa mlangoni kwa babu yake... *Endelea ukurasa wa 2*





Kaburi la mtoto Faston Innocent likiwa limefukuliwa na watu wasiojulikana katika Kijiji cha Katunga, Kata ya Bugombola, wilayani Karagwe, mkoani Kagera jana. **Picha kulia:** Jeneza la mtoto huyo, likiwa limetelekezwa mlangoni nje ya nyumba ya Venant Zabron ambaye ni babu wa marehemu. **PICHA: RESTUTA DAMIANI**

## YALIYOMO


UKURASA WA 14

**VIJUE VIRUSI VINAVYOLINDA MWILI WA BINADAMU, VINAKWEPANA NA BAKTERIA**

KITAALAMU mwilini, kuna kinachoitwa 'microbiome' - makundi ya bakteria...

UKURASA WA 24

**FADLU: KAZI BADO HAIJAISHA**

KOCHA wa Simba, Fadlu Davids, amesema bado...


**Kigogo CHADEMA akamatwa kwa tuhuma za jinai**

UKURASA 2

## Serikali yabeba gharama za mazishi waliouawa Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imegharamia maziko ya miili ya watu wawili kati ya watatu waliouawa katika Kata ya Nala, jijini Dodoma.

Juzi kuliripotiwa tukio la watu watatu, watoto wawili wa familia moja na dada wa kazi, katika eneo hilo.

Waliofariki dunia ni Milcah Robert (12), aliyehitimu darasa la saba katika Shule ya Msingi Chihoni, Fatuma Mohamed (20) na dada wa kazi aliyetajwa kwa jina moja la Micky (16), huku mama wa famili hiyo Lusajo Mwasonge(40) akijeruhiwa.

Mwili wa dada wa kazi ulisa-

**Endelea** Uk. 2


**MICHEZO** **GAMONDI APIGA MAHESABU MAKUNDI CAF** UK 24 **MAONI, KATUNI UK.6**

# Serikali yabeba gharama za mazishi waliouawa Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imegharamia maziko ya miili ya watu wawili kati ya watatu waliouawa katika Kata ya Nala, jijini Dodoma.

Juzi kuliripotiwa tukio la watu watatu, watoto wawili wa familia moja na dada wa kazi, katika eneo hilo.

Waliofariki dunia ni Milcah Robert (12), aliyehitimu darasa la saba katika Shule ya Msingi Chihoni, Fatuma Mohamed (20) na dada wa kazi aliyetajwa kwa jina moja la Micky (16), huku mama wa famili hiyo Lusajo Mwasonge(40) akijeruhiwa.

Mwili wa dada wa kazi ulisafirishwa jana na ndugu zake kwenda mkoani Geita, huku miili miwili ya watoto ikizikwa mkoani Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Msemaji wa familia hiyo, Gwano John, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ndiyo imegharamia baadhi ya gharama za mazishi ya watu hao. Baba wa familia hiyo ni mtumishi wa halmashauri hiyo.

"Msiba huu ni wa kwetu wote tunatangulia kuzika wa hapa Dodoma, mmoja alizikwa jana na tutaondoka na huu mwili mwingine kuelekea Geita kwa kuwa mwili umeharibika na tumezungumza na ndugu muda wowote tutakaofika itabidi tuzike," alisema.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Anania Amo, alisema wanaendelea na uchunguzi wa kuwatafuta waliohusika na tukio hilo.

Ndugu wa dada wa kazi, mkazi wa Kahama, Ramadhan Issa, alisema binti huyo ni mtoto wa kaka yake na walikumbwa na taharuki kutokana na taarifa waliyopokea kueleza kuwa amechinjwa.

"Wazazi walipopokea taarifa za kifo, mazungumzo yaliyoongelewa wakadhani wamesusa kutokana na kukosa taarifa kamili, lakini mwisho wa siku familia ikawa na jazba. Gharama za usafirishaji wengine wakapendekeza miili yote izikwe huku (Dodoma)," alisema.

Alisema kwa taratibu zao, mtu akifariki dunia ni lazima asafirishwe akazikwe nyumbani, kwamba walikutana na mwajiri wake na kukubaliana kuendelea na maandalizi ya kusafirisha mwili.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), Dastan Kamanzi, akitoa elimu kuhusu uandishi wa habari zenye tija kwa Wahariri na Waandishi wa Habari wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), wachapishaji wa magazeti ya The Guardian na Nipashe, katika ofisi za TGL, Mikocheni, Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Kaburi la mtoto lafukuliwa

**Na Restuta Damian,** KAGERA

KATIKA hali isiyo ya kawaida, mwili wa mtoto Faston Innocent (1) umefukuliwa na watu wasiojulikana huko Kahinga, Kata ya Bugomola, wilayani Kyerwa, mkoani Kagera kisha jeneza lake kuwekwa kwenye mlango wa nyumba ya babu yake, Venant Zabron (52).

Akisimulia tukio hilo, babu wa mtoto huyo, Zabron, alisema lilitokea Septemba 17 mwaka huu na kuibua taharuki kwa familia hiyo pamoja na majirani.

Alisema kuwa wakati akiwa ndani ya nyumba yake, alisikia kelele za majirani waliokuwa wakipita kwake lakini hakubaini haraka kilichokuwa kinaendelea.

"Tulipotoka, tuliona jeneza likiwa limefunuliwa na ndani yake kukiwa na mwili wa marehemu mjukuu wangu ambaye tulimzika siku chache zilizopita huku vitu vingine kama mashuka na msalaba vikiwa katika eneo hilo," alisema Zabron.

Alisema kuwa majirani walishangaa huku familia yake nayo ikishtushwa na kitendo hicho kinachodaiwa kufanywa na watu ambao hawakujulikana kwa mara moja.

Zabron alisema kuwa familia hiyo haikuwa na mgogoro wowote ndani ya jamii wanamoishi na hata kifamilia, hata watendwe kiasi hicho.

Kutokana na tukio hilo, baba mzazi wa mtoto huyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa madai ya kuhusika na ufukuaji mwili wa mtoto huyo kwa kile kinachodaiwa kuwa ulizikwa katika eneo ambalo yeye hakuridhia.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kyerwa, Turakira Twijuke, akizungumza na Nipashe jana, alisema kuwa usiku wa kuamkia jana, alipokea mgeni aliyeomba hifadhi huku akidai kutaka kwenda nje ya wilaya kwa ajili ya safari zake za kawaida.

Twijuke alisema kuwa kijana huyo alijitambulisha kwa jina mmoja tu la Innocent lakini baada ya kumhoji ilibainika kuna kitu amefanya na alihitaji kutoroka kwenda nje ili kukimbia suala hilo.

Alisema kuwa ilipofika asubuhi, alianza safari kumpeleka kituo cha polisi lakini baadaye alipokea taarifa za tukio hilo, hivyo kuamua kwenda naye katika eneo la tukio ambako alidai kuwa kijana huyo alizidi kuonesha wasiwasi, hivyo kushukiwa na wakalazimika kumpeleka kituo cha polisi kwa mahojiano zaidi.

"Alipohojiwa alikiri kuwa huyo mtoto ni mwanawe na alizikwa katika eneo ambalo yeye hakuridhia, hivyo akalazimika kutenda tukio hilo kwa lengo la kuishtua familia hiyo itambue kuwa baba wa mtoto hakupendezwa mwanawe kuzikwa katika eneo hilo," alidai Twijuke.

Alisema kuwa baada ya mahojiano hayo, aliachwa kituoni huko kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria na mahojiano zaidi juu ya tukio hilo lililozua taharuki kwa wakazi wa eneo hilo.

Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Bratius Chatanda, ili kuthibitisha tukio hilo na hatua za kisheria zilizochukuliwa lakini hakupatika na kwa kile kilichoelezwa kuwa alikuwa nje ya kituo cha kazi kwa shughuli maalum.

Mkuu wa Kituo cha Kata ya Murongo, Peter Lugenzi, alisema tayari jeshi hilo limechukua hatua lakini yeye hawezi kuzungumzia suala hilo kwa kuwa msemaji ni Kamanda wa Polisi Mkoa.

# Kigogo CHADEMA akamatwa kwa tuhuma za jinai

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema kada wake, Boniface Jacob amekamatwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Itifaki na Mawasiliano ya Mambo ya Nje, John Mrema, alisema kuwa Jacob alikamatwa jana eneo la Sinza na watu waliovalia sare za polisi kisha kumpeleka Kituo cha Polisi Oysterbay.

"Ni kweli Jacob amekamatwa leo (jana) maeneo ya Sinza na watu waliojitambulisha kuwa ni polisi, hivi sasa tumewatuma mawakili wetu waende kufuatilia kubaini nini kosa na taratibu zingine," alisema Mrema.

Alisema kuwa Boniface alikamatwa saa 11:09 jioni, polisi wawili wenye sare na watatu wasiokuwa na sare, wakiwa wamebeba silaha, walifika alikokuwa na kumkamata kwa nguvu na kuondoka naye.

Hata hivyo, kupitia mtandao wa X wa Mrema aliandika: "Polisi wa Osyterbay wanaelekea nyumbani kwa Boniface Jacob muda huu kwenda kufanya upekuzi. Hawajasema wanachokwenda kukipekua, Mawakili wetu wapo na wataambatana naye kuelekea kwenye upekuzi huo."

Taarifa za kukamatwa kwa Boniface ambaye aliwahi kuwa Meya wa Ubungo zilianza kusambaa katika mitandao ya kijamii jioni zikieleza kuwa alikamatwa na askari polisi waliovalia sare, wengine wakiwa wamevaa kiraia waliokuwa na 'defender'.

Jeshi la Polisi kupitia Msemaji wake, DCP David Misime lilithibitisha kumshikilia kigogo huyo wa CHADEMA.

Katika taarifa yake, DCP Misime alisema "Jeshi la Polisi limemkamata na linamshikilia Boniface Jacob, mkazi wa Mbezi kwa Msakuzi, jijini Dar es Salaam kutokana na makosa ya kijinai anayotuhumiwa nayo. Hivyo wananchi wapuuze uongo unaosambazwa mitandaoni kuwa ametekwa."

Mei 6, mwaka huu Boniface, maarufu Boni Yai, alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kujibu mashtaka matatu ya kuchapisha taarifa za uongo kinyume cha sheria. Pia ndiye aliyefichua tukio la ukatili dhidi ya 'Binti wa Yombo Dovya'.

## Muhimbili yapokea vifaa vya upasuaji macho kwa tundu dogo

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imepokea mashine mbili za kisasa zilizogharimu Sh. 68,247,700 kwa ajili ya upasuaji wa macho kwa njia ya tundu dogo kwa wagonjwa wenye tatizo la mtoto wa jicho.

Vifaa hivyo (surgical consumable and medicine na phacoimuisifier) vimetolewa na Vision Care kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA).

Bingwa wa Macho na Mkuu wa Idara ya Macho MNH, Dk. Joachim Kilemile, akizungumza jana jijini Dar es Salaam kuhusu kambi ya mafunzo ya siku tano na kupokea mashine hizo, alisema vifaa hivyo vitarahisisha matibabu, kuokoa muda na mgonjwa kupona mapema.

"Mashine hii ambayo kwa kifupi tunaita 'phaco' itafanya upasuaji kuwa rahisi si mara ya kwanza sisi kufanya upasuaji huu, ila kwa mashine hii itasaidia kufyonza ukungu katika la lenzi na kuweka lenzi nyingine mpya. Mtoto wa jicho maana yake ni lenzi ya jicho imeota ukungu.

"Mashine hii imeongeza ubora kwa sababu awali kwa mgonjwa mwenye mtoto wa jicho alitakiwa asubiri upasuaji hadi mtoto wa jicho akomae.

"Sasa upasuaji hautasubiri hilo atafanyiwa mara tu atakapobainika, kwa gharama ya Sh. 300,000 kwa hospitali binafsi inafikia zaidi ya Sh. milioni mbili," alisema Dk. Kilemile.

Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Vision Care duniani, Dk. Dong Hae Kim, alisema taasisi hiyo imeamua kushirikiana na MNH kwa kutoa mafunzo kwa wataalamu pamoja na kutoa vifaa.

Alisema mafunzo hayo ni pamoja na namna ya kutumia mashine hizo kwa matokeo bora ya matibabu, akisema ni hatua nzuri kwa kuwa vifaa hivyo vimekwishatumiwa kwa miongoni mwa madaktari bingwa wa macho.

Kaimu Mkurugenzi Huduma za Upasuaji MNH, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji MNH, Dk. Ibrahim Nkoma, alisema upasuaji wa tundu dogo utafanyika kwa asilimia 60 hadi 70 na kwamba kati ya wagonjwa 10 wanaohudumiwa miongoni mwao sita watapatiwa huduma hiyo.

"Ninashukuru serikali yetu na Serikali ya Korea Kusini kupitia Vision Care na KOICA kwa kuimarisha huduma za kibingwa na bobezi MNH. "Lengo ni kuwasogezea Watanzania huduma nchini badala ya kuzifuata nje ya nchi kwa gharama kubwa," alisema Dk. Nkoma.

Alisema MNH itawatumia wataalamu wake waliojengewa uwezo kuwapa mafunzo wenzao katika hospitali za kanda, rufani, mikoa na wilaya ili waweze kuwapatia huduma wagonjwa huko waliko.

# Bado siku mbili mbivu, mbichi watakaopata mikopo elimu

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imewataka waombaji wa mikopo yake kwa mwaka 2024/25 kufanya masahihisho kwa wale ambao maombi yao yamebainika kuwa na dosari.

HESLB baada ya kufanya uhakiki wa maombi yao, imebaini baadhi ya maombi yanahitaji kufanyiwa masahihisho ili kuruhusu kuendelea kwa hatua inayofuata.

Taarifa ya HESLB iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa bodi hiyo, Dk. Bill Kiwia, inasema, "Tunapenda kuwataarifu waombaji wote wa Mikopo ya Elimu ya Juu kuwa tunatarajia kufunga dirisha la masahihisho ya maombi ya mikopo ifikapo tarehe 21 Septemba 2024 (keshokutwa) saa 5:59 usiku.

"Wote walioomba mikopo wanashauriwa kuingia katika akaunti zao walizotumia kuomba mikopo kuona iwapo wanahitajika kufanya marekebisho. "Maombi mapya hayatapokewa kwani dirisha la maombi ya mkopo lilifungwa rasmi Septemba 14, 2024.

Makundi ya wanafunzi wanaoomba mikopo ni wanafunzi wa shahada za awali (Undergraduate Degrees); wanafunzi wa Stashahada (Diploma); wanafunzi wa Stashahada ya Juu ya Mafunzo ya Uanasheria (Post Graduate Diploma in Legal Practice); na wanafunzi wa shahada za uzamili na uzamivu (Masters and PhD students).

Bodi hiyo kwa mwaka huu wa masomo imetengewa na serikali Sh. bilioni 787 ambazo zinatarajiwa kuwanufaisha jumla ya wanafunzi 245,000, wakiwamo 80,000 wa mwaka wa kwanza.

Katika mwaka wa masomo 2023/24, serikali ilitoa mikopo kwa jumla ya wanafunzi 224,056, wakiwamo 78,979 wa mwaka wa kwanza.

# Wizara yatoa angalizo chumvi ya upako

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza - Wizara ya Afya, Dk. Omari Ubuguyu, amesema matumizi holela ya dawa yanayofanywa na baadhi ya watu yanachangia ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza ambayo tiba zake ni ghali.

Amesisitiza kuwa kitu kinachoathiri zaidi taifa hivi sasa ni magonjwa hayo na kuwaomba viongozi wa dini kubeba ajenda hiyo ili kusaidia kwa kuwa ni rahisi waumini kuwasikiliza kuliko wataalamu wa afya.

Dk. Ubuguyu aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mafunzo ya viongozi wa dini kuhusu magonjwa yasiyoambukiza yaliyoandaliwa na Chama cha Wagonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA).

"Kwa wale mnaotoa chumvi, mnatoa maji ya upako, mnatakiwa kukumbuka chochote kinachoingia ndani ya mwili kinatakiwa kifanyiwe kazi na kinachofanya kazi ni figo na ini.

"Wengi ambao wameathirika ni kwa kutumia dawa holela wameathiri ini na figo. Jana nilikuwa Hospitali ya Rufani ya Temeke (Dar es Salaam) kuna binti mwenye umri wa miaka 23 yuko katika huduma za kusafisha figo na huu ni mwezi wa pili ameanza matibabu.

"Ndugu zake wanamchangia, amepata msamaha analipa Sh. 150,000, ameshindwa kwenda hospitalini mara tatu kwa sasa anakwenda mara mbili, itafika atashindwa, atakwenda mara moja.

"Nilitaka kujua nini chanzo cha ugonjwa labda ni shinikizo la damu au kisukari, lakini kumbe ni matumizi holela ya dawa," alisema.

Dk. Ubuguyu alisema binti huyo hajawahi kuumwa sukari wala presha bali alikuwa akiumwa kichwa mara kwa mara, hivyo alikuwa akimeza paracetamol na dawa nyingine ili zimsaidie.

"Ghafla akaanza kuona miguu inavimba, akaanza kupata shida katika upumuaji, akaenda Hospitali ya Temeke, alipopimwa figo zikaonekana zimekufa na sasa anaingia kwenye usafishaji figo, maisha yake yote au apate ndugu wa kumchangia figo," alisema.

Dk. Ubuguyu alisema hiyo ni kutokana na matumizi ya dawa kiholela bila kufuata utaratibu wa ushauri wa daktari.

"Dawa za paracetamol zinaathiri figo. Baadhi ya viongozi wa dini wanatoa chumvi wakiwaambia ni upako wakatumie, mwenzako atakwenda kuweka nyingi ili apone na tatizo linakuwa kubwa zaidi, ni muhimu kufanya uchunguzi wa afya hasa wenye magonjwa," alisisitiza.

Alisema mtu ambaye figo hazifanyi kazi kila baada ya siku moja anakwenda hospitalini kusafisha na kila akienda humgharibu kati ya Sh. 200,000 mpaka Sh. 250,000, kwa wiki Sh. 750,000 na kwa mwezi Sh. milioni tatu. Dk. Ubuguyu alisema ameamua kusisitizia hilo kwa sababu watu wanaopata magonjwa wengine wanapona, lakini magonjwa hayo yana tabia ya kuwa katika hali ya chini bila kuonesha dalili zozote.

"Ombeeni watu, toeni maji ya upako, wapeni dawa, lakini wakumbusheni kupima afya zao. Mkiwahudumia warudi kupima ili kuangalia ngazi ya matibabu yao, wahimizeni kuzingatia mtindo bora wa maisha," alisema.

Ofisa Habari Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), John Kamoyo, alisema viongozi wa dini wana wajibu wa kuzungumza na waumini namna ambavyo wanaweza kutengeneza maisha yao kwa sababu hata vitabu vya Mungu vinazungumza juu ya afya njema.

Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Sheikh Hamisi Mataka, alikumbusha kwamba Uislamu umeweka kanuni kwamba, yeyote ambaye atamtibia mtu bila ya kujua maradhi yake anabeba mzigo wa kitakachotokea.

Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza la Viongozi wa Dini Mbalimbali kwa Ujenzi wa Amani Tanzania, Mch. Thomas Muyya, alisema wameitikia wito kuhudhuria mafunzo hayo ili kupata elimu na kuichukua kwenda kuwaelimisha Watanzania kupitia nyumba za ibada.

Shujaa wa kisukari aina ya kwanza, Gaudencia Nyeupe, alisema akiwa chuoni, alianza kuona dalili za kisukari na kwa sababu alishaona wagonjwa wa namna hiyo, alichukua hatua ya kupima na kugundulika anacho na sasa anaendelea vizuri kutokana na kufuata masharti anayopewa na wataalamu wa afya.

Samweli Maingu mwenye tatizo la sikoseli, alisema alichelewa kujua kama anaugua ugonjwa huo kwa sababu ya kukosa elimu, lakini alipogundua ameweza kushinda na sasa anaishi maisha ya kawaida huku akiendelea na masomo yake.


TANROADS

Afrisa Consulting

四川公路桥梁建设集团有限公司

SRBG SICHUAN ROAD AND BRIDGE (GROUP) CORPORATION LTD

**TAARIFA KWA UMMMA**

**KUHAMISHWA KWA BAADHI YA MAKABURI KATIKA BARABARA YA UFI (UBUNGO MAZIWA – SHEKILANGO)**

Mkandarasi wa Mradi wa Upanuzi wa Barabara ya Ubungo-Kimara na barabara shikizi za Morogoro na Kawawa, Sichuan Road and Bridge Group Corporation Ltd (SRBG), anapenda kuutaarifu Umma kuwa anaendelea na ujenzi wa barabara inayopita katika makaburi yaliyopo mtaa wa ubungo kisiwani, Kufuatia ujenzi huu, kuna baadhi ya makaburi yaliyopo kwenye eneo la ujenzi yanahitajika kuhamishwa ili kupisha ujenzi kwenye barabara hiyo.

Hivyo basi tunaomba ndugu wanaohusika na makaburi katika eneo hilo la makaburi ya UFI mkabala na barabara ya Shekilango wafike katika ofisi za serikali ya mtaa, Mtaa wa Kisiwani, Kata ya Ubungo. Kuanzia tarehe 19/09/2024 hadi 26/09/2024

**Tunatanguliza shukrani kwa ushirikiano wenu.**

**Limetolewa na Mkandarasi**
**September, 2024**

IITA Transforming African Agriculture CGIAR

IRRI

## POSITION ANNOUNCEMENT

## ASSISTANT SCIENTIST - Agronomy

### IITA-TZ-2024 - IRRI-011 -NRS

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Rice Research Institute (IRRI) invites applications for the position of **Assistant Scientist - Agronomy**

**Background:** The International Rice Research Institute (IRRI) is a nonprofit independent research and training organization. IRRI is a member of the Consultative Group of International Agricultural research (CGIAR) Consortium.

The Assistant Scientist will assist in the design of experiment(s), survey(s) and other research studies according to Organizational Unit specific project goals and research objectives. Manage the implementation of defined research activities. Evaluate and validate experimental data and contribute to reports and manuscript for peer-reviewed publications as well as presentations/posters for national and international conferences. Supervise, coach and guide scholars, OJTs, researchers and research technicians. Coordinate and prepare training sessions for a variety of stakeholders. Support the agronomy and extension research, promoting rural innovations, partnerships and liaising.

**Duty Station: The position will be based in Bagamoyo.**

**Responsibilities**

**Assist in designing experiments/surveys based on the research outline provided**

- Design, implement, manage and monitor research activities including necessary protocols, research tools, data collection, analysis and interpretation
- Monitor and manage the strategic collaborations around breeding, agronomy and extension research
- Exchange conceptual ideas with collaborating partners (national/international) and seek feedback
- Coordinate with collaborating partners on their research requirements
- Verify suggested methodologies and establish parameters
- Assist in the identification of support staff and assign tasks/responsibilities
- Ensure availability of services and supplies necessary to deliver research objectives

**Manage the implementation of experiments/surveys and other research studies related to breeding and agronomy**

- Provide assistance and guidelines/information to scholars and collaborators considering the implementation of experiment(s) including the logistics
- Assign, monitor and evaluate research activities/tasks performed by Researchers, Research Technicians and contract workers, providing guidance when necessary, for strengthening outreach programs, monitoring, evaluation, action research and experiments
- Maintain smooth conduct of experiment(s) by troubleshooting and fostering a productive teamwork environment
- Develop standard operating procedures (SOPs)

**Consolidate, evaluate and analyze research data**

- Summarize and validate data using appropriate advanced statistical tools independently
- Assist in the interpretation of results
- Assist in drafting conclusions to enable necessary actions or decisions
- Assure maintenance of accurate data recording and update database for efficient storage and retrieval of information

**Contribute to the preparation of reports, publications, and presentations**

- Help draft project reports, prepare posters and papers for presentation at local and international conferences
- Contribute to the development of concept notes and projects for funding or technical collaborations for research and development jointly with relevant IRRI staff
- Develop and contribute towards documentary outputs like knowledge products and research document/ publications/scientific writing/policy briefs, summarizing research findings and draft manuscripts for publication in peer-reviewed journals

**Coordinate and prepare trainings**

- Draft training materials using readily available published information (i.e. protocols, methodology) and also in collaboration with the partners
- Prepare necessary supply; identify resource persons; make sure that the logistics are appropriate for defined purpose
- Responsible for the professional development of Research Technicians

**People Management**

- Supervise the work of Researchers and/or Research Technicians
- Carry out performance appraisals of Research Technicians
- Responsible for the professional development of Research Technicians
- Supervise or assist students and trainees
- Perform other relevant tasks assigned by the supervisor from time to time.

**Key Performance Indicators**

- Successful completion of defined experiment(s) or research studies within given time frame
- Research findings and/or data sets from assigned studies are timely delivered, efficiently generated and a valuable reference for future studies;
- Database is up-to-date, timely and quality reporting and submission of reports to relevant stakeholders
- Presented (paper or poster) to at least one professional conference each year
- Effective monitoring and guiding field technical staff, partner agencies promptly as and when required.
- Satisfactory preparation (material) and set up (supply, venue, logistic) of training sessions as reflected in feedback evaluations

**Qualifications and experience**

- MSc in Agriculture with minimum 3 years of relevant work experience around breeding, agronomy and agriculture extension
- BSc Agriculture with minimum 5 years of relevant work experience around breeding, agronomy, agriculture extension

**Skills and knowledge**

**Mandatory**

- Has proven Technical proficiency in conducting research experiments.
- Has strong oral and written communication skills
- Has strong analytical skills
- Has some experience with Quality assurance
- Has some experience with Research management
- Has good presentation skills
- Has experience on data analysis and relevant statistical tools

**Preferred**

- Working experience in in rice fields

**Languages**

Excellent English and Swahili oral and written skills

**General information:**

**General information:**

The duration of the contract is two years renewable subject to performance and availability of funds. These are nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

The application pack should include an application letter, copies of certificates, and a curriculum vitae which contains a telephone number, email address, and contact details of two referees. Applications should be sent by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org** and addressed to:

The Country Representative, IITA-Tanzania,
Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road,
Mikocheni Industrial Area,
Dar es Salaam, Tanzania

Applicants are requested to include the **reference number for the position** (as indicated on the heading of the announcement) in the subject of their application letter, as well as in the subject of their email. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date for applications: Wednesday 2nd October 2024.**
Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

# ACT Wazalendo, CUF watunishiana misuli

**Na Sabato Kasika**

KATIBU Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ado Shaibu, amegoma kuomba radhi Chama cha Wananchi (CUF) baada ya kutakiwa kufanya hivyo kutokana na kile kilichodaiwa ametoa matusi na kejeli dhidi yao.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, mwanasiasa huyo alisema, "Sitaomba radhi, CUF inakufa kweli. Nimesema tamko la CUF kunitaka kuomba radhi kwa kauli yangu kuwa CUF inakufa na kuwataka wanachama na viongozi wake waliosalia ambao wana moyo wa mapambano kujiunga na ACT Wazalendo. Msimamo wangu ni kuwa sitaomba radhi kwa kauli yangu."

Ado alisema kazi ya siasa ni ya ushawishi, na kwamba ushawishi unafanywa kwa hoja, si matusi wala vitisho, huku akifafanua kuwa tamko la CUF lililotolewa na mkurugenzi wa chama hicho ni ishara ya wazi kuwa "ni taasisi inayokata roho".

"Hakuna taasisi makini ingeruhusu tamko lililosheheni matusi kama lile litoke kwa umma. Binafsi sitaacha kuwashawishi wanachama wa CUF kuja ACT Wazalendo kama ambavyo ninafanya kwa wanachama wa CCM, CHADEMA, wasio na vyama, hiyo ndio kazi ya mwanasiasa. Badala ya kutoa matusi na vitisho, CUF pia wana wajibu wa kufanya hivyo.

"Ninarejea ujumbe wangu kwa wanachama na viongozi wote wa CUF wenye nia ya dhati ya kuendeleza mapambano ya kupigania demokrasia: CUF inakata roho."

Juzi CUF ilitoa taarifa ya kumtaka Ado aombe radhi haraka kutokana na matamshi yanayodaiwa kuwa ya matusi na kejeli dhidi ya chama chao.

Taarifa hiyo iliyotolewa na Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano wa Umma wa CUF, Mohamed Ngulangwa, ilikuwa na madai kuwa kauli ya Ado imeibua taharuki na huzuni ndani ya chama hicho na kwamba haikubaliki.

"Maneno ya Ado ni mwendelezo wa chokochoko za muda mrefu ambazo zimeanza kwa kuvamia mali za CUF, na sasa zimefikia hatua ya kutoa kauli za kudhalilisha mafanikio ya chama chetu," alisema Ngulangwa.

Alisema Ado anajaribu kupandikiza chuki kwa makusudi baada ya ushindi wa CUF katika Uchaguzi wa Mbunge wa Afrika Mashariki kupitia upinzani.

"Taarifa hiyo imebainisha kuwa CUF ni chama chenye misingi thabiti ya haki na uwajibikaji na hakitayumba wala kusalimu amri kutokana na chokochoko zinazojitokeza mara kwa mara," alisema.

Kiongozi huyo alisema CUF ni chama imara chenye mizizi madhubuti ambayo Ado hataweza kuing'oa kwa kuongea mbele ya kipaza sauti kwamba 'CUF imekufa. "CUF pia inatoa onyo kwa Ado, inamtaka aombe radhi hadharani kwa kutumia lugha ya kashfa dhidi ya CUF. vinginevyo chama kitachukua hatua stahiki ikiwa wito huu utapuuzwa," alisema.

# Biteko kuweka jiwe la msingi mradi bwawa kuzalisha umeme

**Na Joyce Lameck**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, leo anatarajia kuwa mgeni rasmi katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme katika Mto Malagarasi, mkoani Kigoma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kaimu Mkuu Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Neema Mbuja, kukamilika kwa bwawa hilo kutawezesha kuzalishwa umeme wa megawati 49.5. Mradi utagharimu Dola za Marekani milioni 144.14 (Sh. bilioni 388).

Alisema kuwa kati ya fedha hizo, Serikali ya Tanzania itagharamia Dola za Marekani milioni 4.14 na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) itagharamia Dola za Marekani milioni 140 kama mkopo wenye masharti nafuu.

Neema alisema mradi huo pia utakuwa na uwezo wa kusafirisha umeme wa kilovoti 132 kutoka Igamba hadi Kidahwe (Km 54) na kituo cha kupoza, kusambaza umeme cha Kidahwe, mkoani Kigoma.

Vilevile, alisema mradi huo utahusisha sehemu kuu tatu; ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme likiwamo tuta, njia ya kupisha maji, nyumba ya kufua umeme yenye uwezo wa kuzalisha megawati 49.5 pamoja na kituo cha kupokea umeme.

Alisema sehemu ya pili itahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 (Km 54) ambayo itaunganisha kituo cha kuzalisha umeme na Gridi ya Taifa kupitia kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe.

Alisema sehemu ya tatu ya mradi huo itahusisha ujenzi wa mtambo wa usambazaji umeme katika vijiji saba, ambavyo vinapitiwa na mradi huo ambavyo ni Mazungwe, Kidahwe, Kalenge, Kazuramimba, Mlela na Igamba.

Alisema umeme utakaozalishwa na mradi huo utasaidia mahitaji ya ndani ya Mkoa wa Kigoma pamoja na kuwezesha biashara ya umeme, huduma za kijamii, ikiwamo elimu, afya, maji pamoja na biashara za viwanda.

## NMB yapiga jeki zahanati

**Na Mwandishi Wetu,**
MAKETE

BENKI ya NMB imekabidhi vifaa tiba, vikiwamo vitanda na mashuka katika zahanati ya Kijiji cha Ivilikinge, wilyani Makete, mkoani Njombe vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni tisa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo mwishoni mwa wiki iliyopita, Kaimu Meneja Benki ya NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Willy Mponzi alisema benki hiyo kila mwaka imekuwa na utamaduni wa kutenga asilimia moja ya pato lake baada ya makato ya kodi kwa lengo la kurudisha kwa jamii.

"Msaada huu ambao leo tumekabidhi Makete pia tumekuwa tunakabidhi katika sehemu mbalimbali katika nchi yetu na huu msaada umehusisha vifaa tiba," alisema Mponzi.

Alisema awali wakati zahanati hiyo inaanza ujenzi, benki hiyo pia ilichangia mabati yenye thamani ya Sh. milioni nane.

Mponzi alisema kuwa kwa miaka kadhaa sasa NMB imekuwa inasaidia miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi kwa kujikita zaidi katika miradi ya elimu ambayo inahusisha madawati, vifaa vya kuezekea.

Benki hiyo pia imekuwa inatoa msaada katika sekta ya afya, ikiwezesha vituo vya kutolewa huduma za afya kupata vifaa kama vile vitanda, magodoro na vifaa vingine vya matibabu.

"Na pia benki ya NMB tumekuwa tukisaidia nchi yetu kwa majanga mbalimbali, tunatambua kuwa ni kupitia jamii ndipo wateja wetu wengi wanakotoka," alisema Mponzi.

Katibu wa Chama cha Maendeleo Makete (MDA), Award Mpandila, alishukuru NMB kwa msaada huo na kuwaomba kuendelea kuboresha uhusiano uliopo kati ya NMB na wananchi.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana alishukuru benki hiyo kwa kuunga mkono jitihada za serikali na wananchi na kuwaomba kuendelea kushirikiana ili kuleta tija kwa taifa.

Awali Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Kijiji cha Ivilikinge, Hassan Yusuph, alisema kuwa baada ya wananchi kuibua mradi wa ujenzi wa zahanati, Benki ya NMB iliwasaidia mabati yenye thamani ya Sh. milioni nane.

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda, aliomba Benki ya NMB kuwaunga mkono pia katika ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa zahanati hiyo.

# Zitto ajitosa madeni ya serikali kwa wasambazaji wa mbolea

**Na Halfani Chusi**

KIONGOZI mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, ameitaka serikali ilipe madeni yote inayodaiwa na kampuni zinazosambaza mbolea ya ruzuku kwa wakulima ili bidhaa hiyo iwafikie kwa wakati.

Zitto alitoa kauli hiyo jana ziarani mikoa ya Njombe na Iringa baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wakulima wanaohofia kuhusu upatikanaji mbolea hiyo kwa wakati kutokana na madeni.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gelard Mweli, alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, alisema "mbolea kwa wakulima ipo, kwanza tuna waingizaji mbolea na mkataba ni kati ya serikali na hao. Je, mbolea ipo au haipo? Inaingizwa au haiingizwi?

"Kuhusu madeni, hiyo ni biashara, kwani sisi hatudaiwi na Benki ya Dunia (WB)? Tunakopa tunalipia na hatujatofautiana na kiasi cha wao kushindwa kuleta mbolea.

"Ingekuwa kuna hali kama wanavyosema wao, wasingeingiza mbolea, kuna mtu anayependa hasara? Kwamba usimlipe halafu aendelee kuleta mbolea? Kwa hiyo, cha msingi mbolea ipo na inawafikia wakulima kwa wakati."

Katika mikutano hiyo kwa nyakati tofauti jana, Zitto aliitaka serikali kuwezesha Kampuni ya Taifa ya Mbolea (TFC) kwa kuipatia mtaji ili ishindane na sekta binafsi, akisisitiza itasaidia kutatua tatizo la ucheleweshwaji wa mbolea.

"Chama chetu tangu mwaka 2022 tulipigania TFC iongezwe mtaji, ili iweze kushindana na wauzaji mbolea binafsi, sekta na kampuni binafsi ili kuleta ahueni, kushusha bei ya mbolea na kupata yenye ubora.

"Jambo la mbolea huwezi kuliachа kwenye mikono ya sekta binafsi peke yake. Tunataka sekta binafsi na umma kupitia Kampuni ya Taifa ya Mbolea washindane kwenye soko," alisema Zitto.

Alisema kwamba wakulima katika mikoa hiyo wamemweleza kuna shida katika upatikanaji mbolea, gharama kuwa juu, ucheleweshwaji na kuwapo mbolea ya ruzuku isiyokuwa na ubora.

Baada ya kusikiliza hoja hizo, Zitto aliahidi chama hicho kitaendelea kupigania suala hilo kupitia Waziri Kivuli wa Kilimo, Mtutura Abdalah, akieleza kuwa tangu kuundwa Baraza Kivuli la Mawaziri, wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha TFC inaimarishwa.

Zitto alisisitiza TFC ndio jawabu la kupambana na bei kubwa ya mbolea na kuhakikisha inafika kwa wakati kwa wananchi.

Alisisitiza kuwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba wanapaswa kuhakikisha madeni ya kampuni zinazosambaza mbolea ya ruzuku kwa wakulima yanalipwa ili kuziwezesha kusambaza mbolea kwa wakati na kupunguza uhaba wa mbolea nchini.

"Tunataka serikali nayo iwajibike, kampuni zinazouza mbolea inayotolewa kwa ruzuku zinaidai serikali mabilioni ya shilingi," alisema Zitto.

Alisema kusuasua kwa mfumo wa usambazaji mbolea za ruzuku kwa wakulima kunateteresha uzalishaji na kufifisha maendeleo ya taifa.

Ziara hiyo ni mwendelezo wa kampeni ya kusajili wanachama milioni 10 kwa miezi 10 na maandalizi kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vijiji.




Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Toba Nguvila (kushoto), akijadiliana jambo na Mkuu wa Idara ya Biashara wa Benki ya NMB, Alex Mgeni baada ya kufungua Tamasha la Kariakoo, lililodhaminiwa na benki hiyo, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapinga Marioo kushinda kesi Korti Kuu, kukata rufani

**Na Kulwa Mzee**

KAMPUNI ya Kismaty Advert Media Ltd imewasilisha nia ya kukata rufani kupinga hukumu ya Mahakama Kuu Masijala Ndogo ya Arusha iliyotupilia mbali shauri lake la kudai Msanii wa Bongo Fleva, Omary Mwana, maarufu Marioo, na meneja wake wailipe zaidi ya Sh. milioni 500 kwa kuvunja mkataba.

Mlalamikaji aliwasilisha nia hiyo baada ya hukumu kutolewa mbele ya Jaji Joackim Tiganga ambapo mahakama baada ya kusikiliza ushahidi iliamua kuitupa kesi hiyo kutokana na kukosekana ushahidi wa kutosha.

Inadaiwa Marioo na Meneja wake, Sweetbert Mwinulan walivunja mkataba wa kutimbuiza katika hafla ya Mr&Miss vyuo vikuu Kanda ya Kaskazini.

Mdai katika shauri hilo, Kampuni ya Kismaty inayojihusisha na kuandaa matukio ya burudani nchini, katika usikilizwaji ilikuwa na mashahidi wanne na walalamikiwa walikuwa na mashahidi wawili.

Mdai anayewakilishwa na Wakili John Lairumbe, anadai kuwa Septemba 23, 2021, aliingia mkataba na wadaiwa kutumbuiza siku ya mashindano hayo kwa gharama ya Sh. milioni 15. Anadai tukio lilitakiwa kufanyika Septemba 24, 2021 Arusha na Septemba 25 mwaka huo ilipangwa kuwa na hafla Blue Stone Lounge.

Kampuni hiyo Septemba 17 mwaka huo iliwalipa wadaiwa Sh. milioni nane na wakati wakitia saini mkataba, iliwalipa Sh. milioni 15.

Inadaiwa Septemba 25, 2021 hawakuonekana kwa ajili ya kutumbuiza Blue Stone kama walivyokubaliana katika mkataba. Kutokana na kuvunja mkataba, mdai aliingia hasara ya Sh. milioni 500,000,000 na hasara nyingine ya Sh. 50,000,000 ambayo ilipatikana kutokana na kukaribisha wadau mbalimbali wakiwamo wamiliki wa hoteli kubwa, fedha walizolipwa na alipoteza biashara na kukosa kipato.

Katika utetezi wao wa pamoja, walalamikiwa kupitia Wakili Clavery Mlowe, walikiri kuwapo mkataba wa utendaji kazi lakini walikanusha kukiuka mkataba na kuongeza kuwa mkataba huo ulitekelezwa kama ilivyokubaliwa Septemba 25, 2021.

Walidai kama kulikuwa na hasara iliyopatikana ilisababishwa na mlalamikaji kwa kutofanya matangazo, hali iliyosababisha wahudhurie watu wachache. Mahakama baada ya kusikiliza pande zote mbili ilitupilia mbali shauri hilo kwa sababu hakuna ushahidi wa kutosha kuthibitisha madai dhidi ya walalamikiwa. Mkurugenzi wa Kampuni ya Kismaty ambayo ndio mlalamikaji, Mary Mollel anadai hakubaliani na hukumu iliyotolewa, anaomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ichunguze kwa kuwa anaona amenyimwa haki yake.

Anadai tangu kesi hiyo ianze mwaka 2021, kumekuwa na figisufigisu nyingi zilizomsababishia kuishi kwa kujificha ndani ya miaka mitatu na kushindwa kufanya kazi zake za kibiashara kama awali.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukatili dhidi ya watoto ulaaniwe, waishi kwa amani

**MATUKIO** mfululizo ya utekaji, watoto kupotea au kukutwa wameuawa na kufanyiwa ukatili wa aina mbalimbali sasa yanajitokeza mara kwa mara na kuleta hofu.

Mfululizo wa matukio haya unaleta sintofahamu kubwa kwa wazazi na walezi.

Hali hii pia imewaibua wadau wapenda haki za watoto na kulaani vitendo vya kutekwa, kuibwa na mauaji ya watoto, wakitaka serikali ichukue hatua kupambana na matukio hayo.

Vitendo hivi vilivyoibuka siku za karibuni vinatafakarisha na kuleta wasiwasi kwa jamii kwa kuwa kila mara lazima zipatikane taarifa za kupotea kwa watoto huku wazazi wakihaha kuwatafuta na wengine kuuawa katika mazingira ya kutatanisha.

Matukio haya yanazidi kushika kasi na jamii kuomba suala hilo kuliweka mikononi mwa Mungu kwa kuwaomba viongozi wa dini kuingilia kati kuliombea taifa liepushwe na upepo huu mbaya unaoanza kuharibu sura ya nchi.

Matukio yaliyowahi kutokea ni la Juni 3, mwaka huu, mkoani Kagera, ambapo mtoto Asimwe Novart, mwenye umri wa miaka miwili, alitekwa akiwa mikononi mwa mama yake na baadaye kukutwa amefariki dunia akiwa amenyofolewa baadhi ya viungo.

Julai 15, mkoani Dodoma, kuliripotiwa tukio la mtoto Sumaiya Issa, kutekwa na mpaka sasa hajapatikana; Julai 7, mwaka huu, huko Mbagala Dar es Salaam, mtoto Nusra Omari alikutwa ameuawa na baadhi ya viungo kunyofolewa; Julai 17 mkoani Dodoma, mtoto Theresphoa Mwakalinga alikutwa amefariki dunia na baadhi ya viungo vyake vimenyofolewa.

Mdau wa haki za watoto kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Getrude Dyabene, alisema anatambua jitihada zinazofanywa na serikali kulinda watoto, lakini wanasikitika kuona ukatili dhidi yao unaendelea.

Kwa mujibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), vitendo hivyo si tu kinyume cha haki za binadamu, bali pia ni kinyume cha Katiba ya Tanzania na sheria za nchi.

"Jeshi la Polisi limekuwa likitolea taarifa matukio ya aina hiyo, hata hivyo haturidhishwi na mikakati iliyowekwa ya ufutiliaji ili kukomesha vitendo hivyo.

"Kwa hali ilivyo sasa tulitarajia Jeshi la Polisi lifuatilie kwa umakini zaidi kujua chanzo cha haya matukio na wahusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua stahiki."

Wadau hao wamewasilisha hoja zao kwa serikali, na walimfikishia Rais Samia Suluhu Hassan, ambapo mdau kutoka Shirika la Msichana Initiatives, Rebeca Gyumi, alimwomba Rais kama Amiri Jeshi Mkuu, aendelee kusisitiza ulinzi na usalama wa mtoto.

"Taasisi zote zenye mamlaka ya ulinzi wa raia zitimize majukumu yake na kukamilisha kwa haraka uchunguzi wa kiini cha matukio haya na upelelezi kwa matukio yaliyotokea."

Kutoka Mtandao wa Haki za Watoto, Msafiri Mwajuma, ameshauri Jeshi la Polisi kufuatilia kwa haraka na kuweka kipaumbele taarifa za watoto kupotea bila kusubiri kupita saa 24.


Katika kufanikisha hilo, wazazi, walezi, jamii, walimu kwa ujumla wametakiwa kuongeza ulinzi kwa watoto na kuwahamasisha kutembea katika makundi, kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi katika jamii na kuwaelimisha watoto wasikubali kuambatana na watu wasiowafahamu.

Hizi ni baadhi tu ya hatua zinazoweza kusaidia watoto kutokumbana na matatizo hayo.

Kwa pamoja suala hili likifanyiwa kazi hakuna kitakachoshindikana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Yasmine Protace

Muungwana Lazima Nilonge

# Wauzaji vyakula jirani na mitaro, mzingatie afya za mnaowahudumia

**MARA** zote kanuni za afya zinajulikana, kwamba unajijali mwenyewe na wenzako, wawe wanafamilia au walio jirani na mahali uliko katika tafsiri pana, kama vile mahali unakofanya kazi zako.

Usafi unatafsiri uhai wa mwanadamu. Hilo lililtumiwa sana na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, katika siku za kwanza za uhuru wa nchi, azma kuu ikiwa kuiunda jamii yenye uhakika na uhai wake.

Mwendelezo wake haujawahi kutelekezwa kitaifa hadi jamii ilikofika, hatua mbalimbali za bidii zinaendelezwa kwenye dhana ya ubora wa afya kitaifa, binadamu wakigawanywa katika makundi mbalimbali kama vile watoto, wazee na kimamama kila kundi na vipaumbele vinavyogusa nafsi zao.

Hali kadhalika, kuna aina ya mazingira yanayojitokeza kitaifa na dunia katika hilo, juhudi za kitaifa zikisaidiwa sana na miongozo ya kimataifa, hasa kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO).

Imekuwa kawaida kila mara tunasikia mlipuko wa magonjwa ama mapya au yaliyokuwa yamejificha na yanaibuka tena. Ndiyo maana hivi karibuni tumekuwa kwenye pilika za kukwepana na maradhi ya corona mitaani kwetu, vivyo hivyo kwingineko duniani.

Tukirejea mazingira ya mahali tuliko na tunaishi, tunashuhudia mvua kunyesha mfano mjini Dar es Salaam, baadhi ya maeneo yenye mitaro imekuwa ikijaa maji, huku wengine wakitumia mvua hizo kuzibua 'chemba' zao za vyoo zilizojaa.

Hata hivyo, katika uhalisi wa maisha, ujio wa mvua ni baraka za asili kutoka kwa Mungu, mvua zisiponyesha, jamii huungana na viongozi wa dini katika maombi ili mvua iweze kunyesha.

Pamoja na hayo, mvua inaponyesha, kuna watu wanaofurahia kupata maji, kwamba ni mbadala wa kununua maji. Pia, wapo wanaopumzika na jukumu la kumwagilia maji bustanini.

Lakini kuna wenzao wanaoangukia vilio, kwamba miundombinu yao inaharibika. Wenye visa hivyo vinawaangukia hata wale Wamachinga, ambao wanaweka bidhaa zao chini na mvua inaponyesha hubomoa utaratibu wote.

Sasa turudi kwa wenzetu wafanyabiashara maeneo ya pembezoni ya mitaro, ambako mvua zikinyesha mitaro kujaa maji, maji hayo hutoa harufu mbaya na kuchangia kuzibuliwa mitaro penye mazingira yao.

Ukiangalia mitaro iliopo pembezoni barabarani kuna wafanyabiashara katika hiyo mitaro iliyozibika, kutokana na uchafu kukusanyika.

Mitaro inapoziba, ambayo ni hali ya kawaida katika sehemu nyingi unakuta mitaro imeziba na wafanyabiashara hawaoni jirani, baadhi kana kwamba hawaoni au wanataabika nalo, wanaendelea na biashara, huku uchafu na harufu yake nayo inaendelea.

Pale mitaro inapozibuliwa, unakuta harufu mbaya inatawala maeneo jirani na kuna mazingira hunishangaza kuona hakuna hisia za wafanyabiashara kukereka, tena wauzaji vyakula na matunda.

Sasa kwa kufanya hivyo kunachangia kuharibu afya ya watu, hasa wateja wa vyakula hivyo.

Napenda niwaeleze ndugu zangu wauza matunda na vyakula, muwe na subira. Kama mitaro imejaa na hali ya afya hapo si salama, jambo jema hasa ni kutafuta maeneo mbadala ya kuendeleza biashara walau kwa muda na sio kuendelea kudumu hapo pasipofaa.

Ila kwa wenye mamlaka, hususan ngazi ya halmashauri, elimu ya kina iendelee kutolewa kwa wahusika kuhusu mustakabali wa afya, maana ndio wadau wenu wa karibu.

Elimu hiyo itasaidia kuwaandaa wafanyabiashara, penye changamoto namna mbalimbali, waliko katika maeneo hayo kibiashara, wajue nini cha kufanya ili kuweza biashara iendelee, sambamba na mazingira mazuri.

Aina hiyo ya ushuhuda si wa watu wazima pekee, pia wanafunzi nao unakuta wamefurika katika vibanda vya wafanyabiashara kunakouzwa milo na vitafunwa, katika mazingira yasiyofaa. Hapo kundi hilo nalo llinahitaji elimu stahiki kutolewa kulinda afya za walaji.

# Serikali yahadharisha uagizaji viyoyozi, majokofu yaliyotumika

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Ashatu Kijaji, amewataka wananchi kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuepuka kuingiza nchini gesi zilizopigwa marufuku na vifaa vinavyotumia gesi haribifu, yakiwamo majokofu na viyoyozi vilivyokwishatumika (mitumba).

Kadhalika, amewataka kuepuka kutupa ovyo majokofu ya zamani ama vifaa vya kuzima moto vyenye kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni au kusababisha ongezeko la joto duniani.

Waziri Kijaji aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni ambayo yanatarajiwa kufanyika Septemba 16, mwaka huu.

Alisema Ofisi ya Makamu wa Rais imepanga kutoa elimu kwa mafundi wa viyoyozi na majokofu katika Jiji la Dodoma kwenye maadhimisho hayo kuhusu namna bora ya kukarabati vifaa hivyo pasipo kuachia angani kemikali na kuharibu mazingira.

Waziri Kijaji alisema kupitia maadhimisho hayo pia wataendelea kutoa elimu kwa umma kupitia makala mjongeo kuhusu umuhimu wa kulinda tabaka la ozoni na kuendelea kuhimiza jamii kupunguza shughuli mbalimbali za kibinadamu ambazo zinasababisha mabadiliko ya tabianchi.

Alisema tabaka la Ozoni kazi yake kubwa ni kuchuja sehemu kubwa ya mionzi ya jua isifike kwenye uso wa dunia.

"Tabaka la Ozoni linapoharibiwa huruhusu mionzi ya jua kufika kwenye uso wa dunia na hivyo kusababisha kuongezeka kwa magonjwa mbalimbali yakiwamo saratani ya ngozi, mtoto wa jicho, upungufu wa kinga dhidi ya maradhi na kujikunja kwa ngozi. Madhara mengine ni kuathirika kwa ukuaji wa mimea," alisema.

Alisema kemikali hizo husababisha kuongezeka kwa joto duniani na hivyo kuchangia katika mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, wataendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi tabaka la Ozoni na kuhamasisha matumizi ya kemikali ambazo ni rafiki kwa mazingira.

"Kutoa mafunzo kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji wa kemikali nchini kwa maofisa wa idara za serikali zilizopo katika Bandari ya Dar es Salaam na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere," alisema.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo imechaguliwa ili kuendelea kujenga uelewa kwa umma namna itifaki ya Montreal imechangia katika hifadhi ya tabaka la Ozoni na kuwa nyenzo muhimu katika kuchangia jitihada za kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.



Mratibu wa Accelerate Africa Tanzania, Pendo Lema (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano wa Accelerate Africa 2024, utakaowakutanisha wajasiriamali kutoka nchi zaidi ya 10 za Afrika, katika Jiji la Arusha Novemba mwaka huu. Wengine ni Mratibu wa Maendeleo ya Vijana wa Accelerate Africa, Isaac Fivawo (kushoto) na Katibu Mtendaji, Jabeen Shiraz. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makundi maalum yaitwa kuomba zabuni serikalini

**Na Romana Mallya**

WAFANYABIASHARA wanawake, vijana na wenye ulemavu wamehamasishwa kuchangamkia fursa za zabuni mbalimbali zilizoko serikalini au mashirika binafsi ili kukuza biashara zao badala ya kuziona kama ni za watu fulani wanaopaswa kuzipata.

Mratibu wa mradi wa kuwajengea uwezo wanawake na vijana kushiriki ununuzi wa umma kutoka Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Julieth Sandi, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya mafunzo ya mradi huo yakiwa na washiriki 30.

Sandi alisema mafunzo hayo ambayo ni ya siku tatu, yameandaliwa na TWCC kwa kushirikiana na Trade Mark East Africa, yakilenga kuwezesha kundi hilo kufahamu fursa zilizoko katika ununuzi wa umma, sekta binafsi na mashirika ya kimataifa.

Sandi alisema mafunzo hayo pia yanalenga kusaidia kujisajili kwenye mifumo ya kidigitali ili kupata fursa elimu kutoka kwa wakufunzi na kuweza kuandaa nyaraka mbalimbali zinazohitajika kushiriki katika ununuzi wa umma.

"Mradi huu ni wa miaka mitatu mwaka 2024/27 umelenga kuwafikiwa wanawake na vijana zaidi ya 1,000 Tanzania nzima. Tutaendelea kufanya mafunzo kwa awamu tofauti katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kati Dodoma.

"Uwezeshaji huu umepewa jina kuwezesha wanawake kushiriki katika fursa zaidi ili kufanikiwa. Pamoja na kwamba wanashiriki, kundi hili limeonekana kukosa uelewa wa fursa za zabuni ambazo zipo serikalini au mashirika binafsi.

"TWCC imeamua kulifanyia kazi suala hili na ndio maana ya kuwapo mradi huu, kwanza wapate ujasiri na washiriki katika zabuni zinazotangazwa," alisema.

Hata hivyo, alisema inawezekana hawashiriki kwa kiwango kikubwa kwa sababu hawajapata elimu sahihi licha ya kuwa na nyaraka muhimu zinazohitajika au kwa kuona kwamba labda kuna watu fulani ndio wanaostahili.

Alisema kupitia mradi huo unakwenda kuwawezesha kuziona fursa hizo na kuzitumia kufanikisha biashara zao.

Meneja wa Kanda ya Pwani wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Vicky Mollel, alipongeza TWCC kwa kuona umuhimu wa kutoa mafunzo ya namna hiyo kwa kundi hilo.

"Wito wangu kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu, tutumie mitandao ya kijamii kuangalia fursa zilizoko na tuzichangamkie. Ingia mtandaoni, angalia fursa leo wamesambaza nini na mimi nitafaidikaje ili kuongeza kipato. Tukumbuke hivi sasa tunakwenda kidigiti, zabuni zinaombwa kidigiti," alisema.

Mollel alisema Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 imeweka fursa nyingi ili kuinua Watanzania, yakiwamo makundi maalum ambapo taasisi za ununuzi zinatakiwa kutenga asilimia 30 ya bajeti zao za ununuzi kwa ajili ya makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, tunahimiza wanawake kuchangamkia fursa zilizoko serikalini. Wanazichangamkiaje kwa kujisajili katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma (NeST)," alisema.

Mfanyabiashara wa chakula, usafi na muziki kutoka mkoani Lindi, Noela Lukanga, ambaye ni miongoni mwa washiriki wa mafunzo hayo, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwao kwa sababu yatawawezesha kukuza biashara wanazozifanya kwa kushiriki kuomba zabuni mbalimbali zinazotangazwa na serikali au mashirika binafsi.

"Mafunzo haya yametufungulia dunia, yametuamsha wanawake wafanyabiashara, kwani yametupa nguvu na mwanga kuona tunaweza kupiga hatua katika kazi zetu. Wito wangu kwa wanawake wenzangu na vijana, tuendelee kujifunza kulingana na dunia ya sasa inavyotaka," alisema.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed





Mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Kibutuka, wilayani Liwale, mkoani Lindi (kulia), akipigwa picha juzi, wakati wa kampeni ya chama hicho ya kusajili wanachama kidigitali, iitwayo 'Jisajili Kielektroniki'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Katibu CCM adaiwa kuuawa na sungusungu

**Na Halima Ikunji,** IGUNGA

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tawi la Ibole, Kijiji cha Ibole, Kata ya Igurubi, wilayani Igunga, mkoani Tabora, Juma Nzera amefariki dunia baada ya kuchukuliwa na kushambuliwa na watu wanaodaiwa kuwa ni jeshi la jadi 'sungusungu' kutoka kijiji jirani cha mkoani Shinyanga, wakidai mtu wao kutoweka akiwa eneo hilo.

Kwa mujibu wa shuhuda wa tukio hilo, Jiganga Jilunga, mkazi wa Kijiji hicho, tukio hilo lilitokea Septemba 13 mwaka huu wakati akichunga ng'ombe katika moja ya malisho yaliyoko kijijini huko.

Alisema kuwa wakati akiendelea na shughuli hiyo, aliona kundi la sungusungu zaidi ya 400 wakiwa na mikuki, fimbo na marungu wakitokea Kijiji cha Ngofila cha wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga.

"Baada ya saa tatu, niliwaona sungusungu hao wakirudi kuelekea kijijini kwao wakiwa wamemtanguliza Juma Nzera (marehemu), nilijaribu kuhoji wanakompeleka na tatizo ni nini, nilijibiwa na watu wawili walionitaka nisirudie kuuliza maswali hayo na ningeendelea wangenishughulikia," alisema Jilunga.

Mtendaji wa Kata ya Igurubi, Michael Kasitu, alithibitisha kuuawa kwa katibu huyo kisha mwili wake kutelekezwa kichakani na kundi hilo la watu wanaodaiwa kuwa sungusungu.

Alisema kuwa baada ya kundi hilo kufika katika kijiji hicho, kulitokea mabishano kati yao na kiongozi huyo, wakidai kuwa kuna mtu wao mmoja amepotea kutoka kijijini kwao, lakini hawakumtaja kwa jina na ndipo waliamua kuondoka na katibu huyo ambaye hakuonekana tena hadi mwili wake ulipookotwa kichakani.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Wilaya ya Igunga, Peter Olonge alithibitisha kutokea kwa mauaji ya kiongozi mwenzao huyo.

Alisema mazishi ya kiongozi huyo yalifanyika juzi Septemba 17 katika Kijiji cha Ibole na kuwa taarifa zimetolewa kwa Jeshi la Polisi ambalo linaendelea na uchunguzi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Costantine Mbogambi, akizungumza na Nipashe alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo, lakini kwa sasa hawezi kuliongelea suala hilo kwa kuwa mauaji hayo hayakufanyika katika mkoa anaosimamia. "Katibu huyo anadaiwa kuuliwa katika Wilaya ya Kishapu, hivyo anayepaswa kulizungumzia suala hilo ni uongozi wa Mkoa wa Shinyanga," alisema Kamanda Mbogambi.

# Uamuzi wa IGP watenguliwa, askari polisi warejeshwa kazini

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masjala Ndogo ya Dar es Salaam imetengua uamuzi wa Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) kuwafukuza kazi askari polisi watatu waliokuwa wanafanya kazi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere baada ya kubaini uamuzi huo ulikuwa ni kinyume cha sheria.

Uamuzi huo wa Mahakama Kuu umetolewa mbele ya Jaji Hussein Mtembwa baada ya kupitia hoja za pande zote mbili, zikiwamo za walalamikaji waliopinga kuondolewa kazini.

Katika kesi hiyo namba 9432 ya mwaka 2024, walalamikaji ni Rabson Mosha (EX G4350 CPL), Amelda Honga (EX. WP 7845 CPL) na Denice Kasimbazi (EX, H5338 D/C) waliokuwa wanawakilishwa na Wakili Peter Majanjara.

Askari hao waliomba kutengua uamuzi wa IGP wa kuwafukuza kazi uliotolewa Oktoba 5, 2023.

Waleta maombi walishtakiwa katika Mahakama ya Kijeshi kwa makosa ya kufanya kitendo kibaya kinyume cha Mwongozo wa Utendaji wa Jeshi la Polisi kwa kumhoji abiria kwa dakika 51, kushawishi na kuchukua fedha za rushwa kutoka kwa abiria.

Wajibu maombi katika shauri hilo ni IGP na Mwanasheria Mkuu wa Serikali waliowakilishwa na Wakili wa Serikali Doreen Muhina.

Wakili Majanjara alidai kuwa kulikuwa na ukiukwaji utaratibu kwa kutozingatia upelelezi wa awali wa makosa yaliyowakabili waleta maombi.

Alidai wajibu maombi walishindwa kuzuia adhabu ya kuwafukuza kazi wakati wamekata rufani, kwamba kosa la kufanya kitendo kibaya kinyume na mwenendo mwema wa Jeshi la Polisi kwa kuhoji abiria kwa dakika 51 halikuwa kosa kwenye sheria yoyote na lilitengenezwa ili kuwaondoa waleta maombi kazini.

Alidai makosa dhidi ya waleta maombi hayakuthibitishwa kwa mkanganyiko kwenye ushahidi na kukosa ushahidi. Pia wajibu maombi walinyimwa ripoti ya uchunguzi na mwenendo wa kesi dhidi yao.

Wakili Muhina, akijibu hoja, alidai waleta maombi waliwasilisha maombi mapya ambayo hayakuwapo kwenye kiapo chao, kukiwamo kutosimamisha adhabu ya kufukuzwa kazi wakati wamekata rufani na kwamba upelelezi wa awali dhidi ya waleta maombi ulifanyika.

Alidai kwamba makosa dhidi ya waleta maombi kutothibitika, mahakama haina mamlaka kuingilia ushahidi bali kuangalia uhalali wa uamuzi wa chombo cha umma.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja, ilisema kwamba kisheria, wajibu maombi walipaswa kuweka mwenendo wa shauri dhidi ya waleta maombi na kuwapatia nakala, lakini hawakufanya hivyo.

Julai 31, mwaka huu, mahakama iliwaamuru wajibu maombi kuwasilisha mwenendo huo lakini waleta maombi hawakupewa.

"Chombo chochote cha umma kinacholalamikiwa kuhusu uamuzi wake kinawajibika kuleta nyaraka zote zinazohusiana na malalamiko kwa sababu wao ndio wana nyaraka zote za kusaidia mahakama kwenye kuamua kuhusu malalamiko yaliyopo mbele yake.

"Hata kwenye kesi tofauti tofauti, mahakama zimekuwa zikitengua uamuzi wa vyombo vya umma pale ambapo vinashindwa au kukataa kuwapatia waleta maombi mwenendo.

"Mahakama inaona kwamba wajibu maombi waliamua kutengeneza muhtasari wa mwenendo wa shauri dhidi ya waleta maombi bila kuwapo kwao," alisema Jaji.

Alisema mahakama ya kijeshi ilipowakuta waleta maombi na hatia ya makosa dhidi yao, walimwachia Kamanda wa Viwanja vya Ndege (ASP Jeremia Shila) ambaye haonekani akitoa adhabu yoyote kwa waleta maombi lakini akaendelea kuwafukuza kazini.

"Kwa wajibu maombi kushindwa kuleta mwenendo kamili na kuonesha adhabu iliyotolewa, inaonesha kwamba hakukuwa na adhabu yoyote dhidi ya waleta maombi.

"IGP hakutakiwa kutoa uamuzi kwenye rufani ambayo haikuwahi kutolewa uamuzi wa awali, ni sawa na kusema kwamba Jeshi la Polisi halikuwahi kuwaadhibu waleta maombi, mpaka sasa wametiwa tu hatiani kwa makosa dhidi yao.

"Kwa kusema hayo, mahakama inaamuru uamuzi wa IGP ni kinyume cha sheria, uamuzi wa kuwafukuza waleta maombi umetenguliwa," alisema Jaji Mtembwa.

# Mafundi ujenzi wawachongea wafanyabiashara kwa 'bosi' TRA

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAFUNDI ujenzi wilayani Kahama, mkoani Shinyanga wamemweleza Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda, namna wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi wanavyokwepa kodi kwa kuwapatia risiti ambazo haziendani na ununuzi waliofanya na kuwa wanapohoji hawapati majibu sahihi.

Mwenyekiti wa Mafundi Ujenzi wilayani hapa, Baraka Mushi alibainisha hayo juzi wakati wa kikao kazi cha Kamishna Mkuu wa TRA na wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa ambacho ni sehemu ya kujitambulisha kwao na kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili ili kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema wafanyabiashara wanaouza vifaa vya ujenzi wanaongoza kwa kukwepa kodi kulinganisha na makundi mengine kwa kuwa wanaponunua vifaa wanapewa risiti za kielektroniki ambazo hazioneshi uhalisia wa bei ya mali iliyonunuliwa na wanapohoji wanatishiwa kunyang'anywa mzigo; kwa kuwa hawana namna wanakubali.

"Kamishna Mkuu, kitendo hiki kinachofanywa na wafanyabiashara wetu kinatuumiza na inatufanya kuonekana nasi ni miongoni mwa wakwepakodi, na kama kuna mfumo wowote unaweza kutufanya tukalipa kodi, tuko tayari kulipa ili tuwe miongoni mwa wazalendo wa nchi hii wanaolipa kodi na si kukwepa kodi," alisema Mushi.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara, Charles Machari aliahidi kufutilia kujua uhalali wa utoaji risiti ambazo haziendani na mali iliyouzwa na atatoa taarifa haraka na wale watakaobainika watachukuliwa hatua za kinidhani kwa kuwa watakuwa wanawachafua wengi wanaotambua umuhimu wa kulipa kodi.

Kamishna Mkuu wa TRA, Mwenda, aliwapongeza mafundi ujenzi kwa kufichukua siri hiyo na kuwataka pale inapotokea shida hiyo na nyinginezo za kikodi, kufika ofisi za TRA na kutoa taarifa ili wawashughulikie kisheria.

Alisema Kahama ina zaidi ya wafanyabiashara 24,000 waliosajiliwa na TRA na watambulika na hao ndio wanaofanya wilaya hiyo kufanya vyema kwenye ukusanyaji kodi kulinganisha na mikoa mingine.

"Sasa inapoanza tabia ya kukwepa kodi kwa kutoa risiti ambazo si sahihi... watakaobainika watawajibika," alionya Kamishna Mkuu.



# Mchengerwa atoa maagizo 3 kwa ma-RC, DC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa, amewaagiza wakuu wa mikoa, wilaya na viongozi wa halmashauri kusimamia utambuzi wa awali wa watoto wenye mahitaji maalum.

Vilevile ameagiza viongozi hao kuunda mikakati ya kuwalinda watu wenye ulemavu wa ngozi, ili kudhibiti matukio mbalimbali ya ukatili wanayofanyiwa.

Alitoa maagizo hayo jana jijini Arusha, wakati wa kufungua Maadhimisho ya Miaka 30 ya Elimu Jumuishi nchini, yaliyofanyika Shule ya Elimu Jumuishi ya Patandi iliyopo wilayani Arumeru.

Aidha, aliagiza kutumia vituo na wataalamu wa uchunguzi waliopo katika halmashauri, ili waweze kuwaelekeza katika shule stahiki au sehemu stahiki, ambazo wanapaswa kupelekwa kupata afua stahiki.

Alisema zoezi la kubaini watoto hao wenye mahitaji maalum, lifanyike kabla ya kipindi cha uandikishaji kwa kufuata miongozo ya utekelezaji wa zoezi hilo iliyotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI mwaka 2022, ile iliyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mwaka 2023.

"Ma RC, DC na viongozi wa halmashauri anzeni zoezi la kuhakikikisha watoto wenye ulemavu wanatolewa nyumbani na kwenda shule na wale wanaowaficha watoto hawa wabainike, lakini wanaofanya ukatili kwa watoto wenye ulemavu wa ngozi wachukuliwe hatua mara moja," alisema.

**"Hakikisheni vituo vya Huduma ya Upimaji na Uchunguzi wa Kielimu (ESRAC) kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum vilivyopo kila mikoa na halmashauri vinaimarishwa..."**

Alitoa rai kwa wazazi na walezi kuhakikikisha wanawapeleka watoto wenye mahitaji maalum katika shule zilizoshauriwa na wataalamu, ili wakaandikishwe na kuanza masomo.

"Hakikisheni vituo vya Huduma ya Upimaji na Uchunguzi wa Kielimu (ESRAC) kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum vilivyopo kila mikoa na halmashauri vinaimarishwa kwa lengo la kutoa huduma stahiki," alisema.

Alisema awali baada ya uhuru kulikuwa na wanafunzi wenye mahitaji maalumu wachache shuleni lakini hadi kufikia mwaka 2020 kulikuwa na wanafunzi wenye mahitaji maalumu 28,482 katika shule mbalimbali.

Alisema lakini kutokana na sera, miongozo na mikakati iliyoandaliwa, imeongeza watoto hao na kufikia wanafunzi 78,429 mwaka 2024.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2021/ 2024 serikali imejenga mabweni 172 kwa kutumia mfuko wa serikali kuu pamoja na miradi mbalimbali, vyumba vya madarasa 44 na matundu ya vyoo 132.

Pia, alisisitiza walimu wanaofundisha wanafunzi hao kupewa motisha na changamoto zao kushughulikiwa mara moja ili waweze kutoa elimu kwa watoto hao.

Mkurugenzi wa Idara ya Elimu Maalum, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk.Magreth Matonya, alisema maadhimisho hayo yanalengo la kuhakikikisha maadili, ujuzi, ubunifu na teknolojia ni kwa ajili ya kuwawezesha watoto hao, kuhakikikisha wanaweza kujiajiri pindi wamalizapo shule.



Polisi Kata wa Kilulu, wilayani Muheza, mkoani Tanga, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Charles Furahini Mbaga, akitoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Kilulu jana, kuhusu kupinga vitendo vya ukatili na kutoa taarifa pindi watakapoona wanafanyiwa ukatili. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mitaa 60, kata 21 Moshi kutumika uchaguzi S/mitaa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HALMASHAURI ya Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, imesema Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, utahusisha mitaa 60 na kata 21 na pekee.

Hivyo, amewaonya wanasiasa kutowayumbisha wananchi kuhusiana na mipaka ya maeneo ya kiutawala yanayotambuliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Onyo hilo lilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa hiyo, Mwajuma Nasombe, wakati akitangaza mipaka ya maeneo ya uchaguzi.

Katika taarifa yake, aliwataka viongozi wa siasa na watendaji wa serikali, kuhakikisha wanatoa elimu sahihi kwa wananchi.

"Halmashauri yetu ya Manispaa ya Moshi, imejipanga kushiriki vyema katika zoezi la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuchagua viongozi wenye sifa.

Juzi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alitangaza amri na notisi (ilani) ya mgawanyo wa maeneo ya kiutawala katika serikali za mitaa, akisema kuna mitaa 4,269 na vitongoji 64,274 imerejeshwa kwenye maeneo ya kiutawala nchini.

Pia, alisema serikali imerejesha takwa la kikatiba kwa wakazi wa Ngorongoro, mkoani Arusha na maeneo mengine nchini, kushiriki upigaji kura kwenye maeneo ya kiutawala ya vijiji 12,333 vilivyokuwa vimefutwa.

# Mkuu wa Mkoa atoa onyo watakaovuruga uchaguzi

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani, ametoa onyo kwa wananchi watakaokwenda kinyume na taratibu za uchaguzi kwa kufanya mambo yanayoweza kuwatia hatiani katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

Alitoa onyo hilo jana jijini hapa, wakati akiainisha makosa yatakayomtia hatiani mwananchi au mjumbe yeyote anayegombea katika uchaguzi huo.

Aliyataja baadhi ya makosa ni endapo mwananchi ataharibu orodha ya wapigakura au nyaraka zozote zinazohusiana na uchaguzi, endapo atatoa taarifa za uongo kuhusu uraia wake, lakini kama atajiandikisha zaidi ya mara moja ikiwa ni pamoja na kupiga kura zaidi ya mara moja kwa wagombea wa nafasi moja.

Alisema kosa lingine ni kutishia wapigakura au wagombea ili kuvuruga uchaguzi, lakini pia kufanya kampeni siku ya uchaguzi, kuonesha ishara au kuvaa mavazi yanayoonesha yanayomtambulisha mgombea au chama cha siasa mita 200 kutoka kwenye kituo cha kupigia kura.

Alisema kosa lingine ni kumzuia msimamizi wa uchaguzi au msimamizi wa kituo atakayeteuliwa kutekeleza majukumu yake, kukiuka masharti ya kiapo chake, kupatikana kwa karatasi ya kupigia kura zaidi ya moja kwa nafasi moja aliyogombea.

Lakini pia, alieleza mtu asiye na dhamana, endapo atatangaza matokeo ya uchaguzi kabla hayajatangazwa rasmi na msimamizi wa uchaguzi.

"Makosa haya yanapotokea na mtu yeyote atakayepatikana na hatia za kosa lolote la uchaguzi atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi Sh. 300,000 au kifungo kisichozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja.

Alisema: "Hivyo ni vizuri wananchi wakajua makosa haya ili wasije kujikuta kwenye matatizo bila kujua, wito wangu kwa wakazi wa Mkoa wa Tanga, ninawasihi sana wote wenye umri wa kuanzia miaka 18 au wale watakaofikisha umri huo siku ya kupiga kura". Hivyo, aliwataka wananchi kujiandikisha tena kwenye Daftari la Mpigakura ifikapo Oktoba 11, ili wasipoteze haki ya kuchagua viongozi wanaowahitajika.

Baadhi ya wananchi waliiomba serikali kuboresha huduma kwenye vituo vya kujiandikisha na kupigia kura, ikiwa ni pamoja na muda wa kujiandikisha uongezwe wakisema siku 10 pekee hazitatosha.





# RC ashangaa Shinyanga kukosa kiwanda cha maziwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amesikitishwa na kutokuwapo kwa kiwanda cha kusindika maziwa mkoani humo licha ya kuwa na wafugaji na mifugo mingi.

Alibainisha hayo juzi wakati wa uzinduzi wa Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia mkoani humo, ambayo inasimamiwa na Ofisi ya Rais Ikulu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC).

Alisema kupitia programu hiyo wananchi wanapaswa kuchangamkia fursa za kiuchumi zilizoko mkoani humo, ikiwamo kuanzisha kiwanda cha kusindika maziwa.

"Suala linalosikitisha zaidi ni kuwa ukienda madukani unakuta maziwa yaliyosindikwa kutoka Tanga, Iringa, Mara, Kilimanjaro, lakini hakuna maziwa ya hapa Shinyanga," alisema Macha.

Mshauri wa Rais Samia masuala ya wanawake na makundi maalumu, Sophia Mjema, alisema dhamira ya Rais ya kuanzisha programu hiyo, amelenga kuwainua wananchi wote kiuchumi na hakuna ambaye ataachwa na wala hakuna kuingiza vikundi kwenye kanzi data kwa urafiki na hata kujuana.

Alisema Rais Samia amewatuma kufufua majukwaa yote ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo yalikuwa yamelala, ndiyo maana wanazunguka mikoa yote, ili kutambulisha programu ya imarisha uchumi na Mama Samia, kwa kukutana na viongozi pamoja na makundi ya wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum.

Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'i Issa, alisema hatua ya kwanza ya programu hiyo itahusisha uandaaji wa kanzi data ya walengwa, utambuzi wa shughuli za kiuchumi za uwezeshaji, kwa vikundi vilivyotambuliwa au sajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalumu.

Alisema: "Tumelenga kuwafikia wanufaika 62,000 na hadi sasa tumevuka lengo tumefikia wananchi 70,000 na hii inaonyesha mwitikio ni mkubwa."

Aidha, alisema katika programu hiyo watafufua vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi, kwamba kwa sasa vipo 25 nchini.

# Mwigulu awaita w'biashara kuwekeza Kanda ya Ziwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba amewataka wafanyabiashara Kanda ya Ziwa kuchangamkia fursa za kibiashara katika Soko Kuu la Kisasa la Mwanza, ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 96.

Alitoa wito huo juzi jijini hapa baada ya kufanya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa soko hilo, ambako alieleza kuridhishwa na hatua iliyofikiwa na kusema utekelezaji wake umezingatia viwango vya kimataifa na matakwa ya kimkataba.

"Mkataba uliopo baina ya wananchi na serikali ni kuhakikisha tunawaletea maendeleo kwa kutekeleza shughuli na miradi mbalimbali ya kimaendeleo ambavyo ndicho kitu tunachokifanya kwa sasa, hivyo wajiandae tu kuanza kupata matunda ya mradi huu muhimu katika uchumi wa Kanda ya Ziwa," alisema.

**"Likikamilika soko hili pekee tunatarajia kukusanya zaidi ya Sh.bilioni 3.7 kwa mwaka na pia utekelezaji wake umetoa ajira kwa vijana 175 ambao pia wanaendelea.."**

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Erick Mvathi alisema umefikia asilimia 96 na zaidi ya Sh. bilioni 21 zimelipwa kwa mkandarasi pamoja na fedha za madai ya utekelezaji kwa wakati.

Alisema soko hilo kwa ujumla linatarajiwa kutumiwa na wafanyabiashara zaidi ya 1,400, huku kilichosalia ni pamoja na sehemu ya kuhifadhia taka, kupaka rangi, utengenezaji wa mifumo ya maji pamoja na mifumo ya umeme.

Aidha, alisema soko hilo lina maduka makubwa na madogo 514, vizimba 332, maeneo ya kuuzia samaki 372, vizimba vya machinga 167 pamoja na eneo la kuegesha magari 192.

"Likikamilika soko hili pekee tunatarajia kukusanya zaidi ya Sh.bilioni 3.7 kwa mwaka na pia utekelezaji wake umetoa ajira kwa vijana 175 ambao pia wanaendelea na utekelezaji wake," alisema Mvathi.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alisema wamepokea zaidi ya Sh.bilioni 350 ambako Sh.bilioni 111 ni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Meli ya Mv. Mwanza Hapa Kazi Tu.

Alisema Sh.bilioni 23 ni kwa ajili ya soko kuu, stendi kuu ambayo imegharimu Sh.bilioni 17 pamoja na utekelezaji wa miradi ya barabara Sh. bilioni 11.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba anaendelea na ziara yake ya kikazi mkoani Mwanza kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo pamoja na kuwela mawe ya msigi pamoja na kufanya mikutano ya hadhara.

Miradi huo unatekelezwa na mkandarasi Mohamed Builders kwa Sh. bilioni 23.3 pamoja mkandarasi mshauri OGM Consultant ambaye analipwa Sh.bilioni 2.8 ulianza kutekelezwa Septemba 30, mwaka 2019.

Hata hivyo, ujenzi wake ulisimama kutokana na sababu za kifedha, hali ya kijiografia pamoja na usambazaji wa vifaa uliokwamishwa na janga la ugonjwa wa corona, ulitarajia kukamilika Aprili, 2022.

Inaelezwa kuwa kutokana na changamoto ya malipo kwa mkandarasi mradi huo haukukamilika kwa wakati, hivyo mkandarasi kuomba kuongezewa muda hadi Machi 25, mwaka huu.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkandarasi Mshauri kutoka Kampuni ya OGM Consultants, Mhandisi Henry Chundu (kushoto), kuhusu mradi wa Soko Kuu la Mwanza, alipotembelea na kukagua ujenzi wake juzi, uliofikia asilimia 96 na kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 23.3. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Bashe aagiza kutengwa eneo la kuuzia tumbaku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, Hadija Kabojela, kutenga eneo litakalotumika kama soko wakati wa mauzo ya tumbaku.

Amesema lengo ni kuondoa adha ya wakulima kukimbilia mkoani Tabora kuuza zao hilo na kusababisha halmashauri hiyo kukosa mapato.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wananchi na wakulima wa mazao ya chakula na biashara katika Kijiji cha Mbika Kata ya Ushetu.

Alisema mkurugenzi anatakiwa kutenga eneo mahususi kwa ajili ya soko la tumbaku na serikali iko tayari kujenga maghala matatu makubwa yatakayotumika kuhifadhi zao hilo, akisema itasaidia kuwadhibiti wakulima wanaotorosha tumbaku.

Bashe alisema ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, serikali inatarajia kujenga mabwawa matatu makubwa katika Kata ya Kisuke, Nimbo na Bulungwa-Butibu yatayotumika katika kilimo cha umwagilia.

"Kwenye shamba la kisuke ambalo litakuwa na ukubwa wa hekari 833 tutaweka mradi wa BBT ili kunufaisha vijana na kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Tutaleta trekta 10 yatakayotumiwa na wakulima pamoja na kokodishwa kwa hekari moja Sh.35,000 badala ya Sh.60,000 iliyopo sasa," alisema.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa vyama vya msingi (Amcos) kuhakikisha vinafunga mkataba wa miaka mitatu na kampuni inayonunua zao hilo, ili kuhudumiwa kwa pamoja, kujengewa mabani ya kisasa na kupata pembejeo kwa wakati.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Charahani, aliomba serikali kuondoa tozo ya miti kwenye kilimo cha tumbaku ili kupunguza gharama za uzalishaji.

ama

ALHAMISI SEPTEMBA 19, 2024

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**STAILI NNE ZA MIUNDOMBINU...**
**Simulizi ya miaka mitatu ya Awamu VI, ilivyopokea MMAM kwa mtaji majengo**



**Vijue virusi vinavyolinda mwili wa binadamu, vinakwepana na bakteria**

Ukurasa 14

## KILICHOWABEBA RAIS AKAWASIFIA...

# Mapinduzi maji Tanga kutoka hatari ukame, hadi mwelekeo kujitosheleza

## •Dk. Mpango naye, 'mfano kuigwa kujitegemea kifedha'

**Na Cheji Bakari, TANGA**

MIONGONI mwa vivutio vikubwa katika mazingira, ni uwapo wa vyanzo vya maji vya aina mbalimbali na kwa wastani mkubwa, ndio unajenga maisha ya mwanadamu.

Na inapotajwa dhana ya vyanzo vya maji, ni maeneo yote ambayo maji huanza, kabla ya kusafiri kwenda sehemu nyinginezo.

Mkoani hapa hivi karibuni, Kamati ya Kudumu ya Bunge Maji na Mazingira ilifanya ziara ya siku moja mkoani Tanga ilitembelea Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga UWASA lengo ni kukagua jinsi fedha zilizotolewa na serikali kutekeleza miradi ya maji.

Kamati hiyo, pia ilitembelea na kukagua idara mbalimbali za mamlaka hiyo, ikiwamo Bwawa la Kuhifadhi Maji la Mabayani linalokusanya maji kutoka chanzo kikuu cha Mto Zigi, unaoanzia milima ya Usambara - Tao la Mashariki katika Tarafa ya Amani wilayani Muheza.

Pia, ikatembelea Kituo cha Kutibu na Kusafishia Maji cha Mowe, vyote katika Kijiji cha Pande, nje kidogo ya Jiji la Tanga.

Katika ziara hiyo, kamati ilivutiwa na jinsi mamlaka hiyo ilifanikisha mpango wake wa kuvilinda na kuvitunza vyanzo vyake vya maji ikiwa na faida nyingi jamii kwa jamii inayoishi kandokando ya vyanzo hivyo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jackson Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, anasema kamati yake imefurahishwa na mpango huo, ambao mamlaka hiyo inatunza rasilimali maji.

" Sisi kamati kazi yetu ni kuhakikisha wananchi wanapata maji, kupitia fedha mbalimbali zilizotolewa na serikali na zile za hatifungani, ili kutimiza falsafa ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani," anatamka Kiswaga.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA), Mhandisi Geofrey Hilly (wa pili kushoto), akitoa maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge Maji na Mazingira. Kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian. **PICHA: CHEJI BAKARI**

### UWASA INAVYOWAJIBIKA

Katika hatua zake kukabili uhaba wa maji, UWASA ilianzisha afua mbalimbali za kutunza vyanzo vya maji, ikiwamo katika Mto Zigi, baada ya watu kuvamia chanzo cha mto huo katika Milima ya Usambara, lengo lao ni kutafuta madini ya dhahabu.

Shughuli hizo kwa asilimia kubwa, zilisababisha uchafuzi wa mazingira na kupunguza kina cha maji katika mto huo, hali ambayo wadau wa mazingira waliingilia kati kwa kuanzisha afua mbalimbali za kuhifadhi mazingira.

Hiyo ikaendana na kuweka ulinzi shirikishi na kutoa elimu kwa jamii ya vijiji vinavyozunguka mto huo jinsi ya kutunza mazingira.

Namna ilivyofanikisha, ilianzisha vikundi vya wakulima na Wahifadhi Mazingira Kihuhwi na Zigi (UWAMAKIZI), waliowapa elimu jinsi ya kufanya kilimo rafiki wa mazingira, pasipo kuathiri vyanzo vya maji.

Ilikuwa ni zao la elimu waliopewa, hata wananchi wananchi walijiunga katika vikundi na kulima mazao ambayo ni rafiki wa mazingira, hata yamenufika upande huo kiuchumi.

Pia, faida nyingine jambo hilo limeongeza kina cha maji, kupunguza tope mtoni pamoja na uchafuzi wa maji ambapo ilifanya mamlaka hiyo kutumia fedha nyingi kununua kemikali za kusafisha maji kabla ya kuwapelekea wateja jambo ambalo iliwalazimu kuongeza fedha za ankara za maji.

Katika utekelezaji wake, ni kwamba kukawekwa mawe ya mipaka inayozunguka bwawa la Mabayani, linalokusanya maji kutoka chanzo kikuu cha Mto Zigi, ili kuzuia shughuli za kibinadamu.

Mafanikio hayo yameifanya serikali kuipa majukumu mamlaka hiyo kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kwa mkoa huo, ukiteuliwa kuwa mkoa wa kimkakati, ikibashiriwa idadi ya wakazi itazidi kuongezeka.

### WAZIRI WA MAJI

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ambaye pia ni mbunge mkoani hapa, anasema tayari mamlaka hiyo imeshatia saini mikataba na makandarasi wawili kuboresha mtandao wa majisafi na taka katika jiji la Tanga, baada ya kupata takribani shilingi bilioni 54, kupitia Hatifungani ya Kijani.

Anasema mradi huo unatarajiwa kukamilika mapema mwezi Oktoba mwaka ujao, ikiongeza lita kati ya milioni 45 hadi milioni 60 ya maji ukinufaisha watu 600,000.

"Hizi fedha za hatifungani zinatarajiwa kunufaisha wakazi wa maeneo ya miji ya Tanga, Mkinga, Muheza na Pangani..." anasema.

### UPATIKANAJI MAJI

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Batilda Burian, anasema maji yanapatikana kimkoa, kati ya asilimia 59 hadi 60 kwa wilaya zote nane za mkoa huo na dira ya serikali ni kuhakikisha hadi mwakani maji yaopatikane kwa asilimia 95 ya mahitaji mijini na vijijini asilimia

Inaendelea Uk. 14

AFYA

STAILI NNE ZA MIUNDOMBINU...

# Simulizi ya miaka mitatu ya Awamu VI, ilivyopokea MMAM kwa mtaji majengo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kunaanza Awamu ya Sita ya Uongozi wa Serikali chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mnamo Machi 2021, kuliendana na mikakati ya 'papo kwa hapo' kuboresha maendeleo ya nchi ipige hatua zaidi.

Mara moja hatua yake ikaendana na kutumikia maelekezo kutoka Ilani ya chama chake - CCM, ikibeba ujumbe wa sekta ya afya: "Ongezeko la vituo vya kutoa huduma za afya nchini na maboresho ya miundombinu..."

Kimsingi, ni aina ya ufafanuzi wenye haja ya kuwezesha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, umbali wa kilomita tano kutoka waliko ifikapo mwaka 2025 na itakapofika mwaka 2030, iwe asilimia 95 ya kundi hilo.

Vilevile, katika sura ya pili Awamu ya Sita ya uongozi wa Rais huyo inaendana na uamuzi wa kuwekwa mitambo 21 hospitalini kuzalisha hewa tiba ya oksijen, kwa wagonjwa mahututi na wenye dharura.

Vyote ni uendelezaji wa yaliyoasisiwa na Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Rais Dk. Jakaya Kikwete - Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ulioasisiwa mnamo Julai mwaka 2007 na kuanza kazi rasmi, mwezi kama huo mwaka uliofuata.

Kwa mujibu wa MMAM iliyopo kisheria, kila mtaa mjini au kijijini inakuwa na zahanati, kata kuwa na kituo cha afya, wilayani kuna hospitali, mikoa na hospitali za rufani, hali kadhalika juu yake hospitali za rufani za kanda na ngazi ya juu zaidi ni hospitali za taifa, ikiwamo Muhimbili (MNH), ambayo ina tawi lake la Mloganzila, Dar es Salaam.



Rais Samia alipokuwa mjini Mpanda, kuzindua Hospitali ya Mkoa Katavi, Julai mwaka huu.

**UJENZI MIUNDOMBINU**

Rais Dk. Samia, katika eneo ambako kuna uwekezaji miundombinu wa kina katika fursa za matibabu, inagawanyika katika sura tatu, ambayo eneo linaloacha kwa kina mlipuko wa fursa nyingi za matibabu kitaifa, hata kuweka rekodi mpya.

Ni aina ya ujenzi katika miaka hiyo mitatu ya Rais Dk. Samia, unaogusa sura za kuendeleza ujenzi katika hospitali mpya tano za rufani katika mikoa mitano; Katavi, Njombe, Songwe, Simiyu na Geita, ikigusa sura za majengo mapya, ukarabati na kukamilisha miundombinu yake.

Aidha, katika sura nyingine inayofanana na hiyo, inagusa kukamilishwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani Kanda Kusini Mtwara na Awamu ya Pili ya Hospitali Chato.

Vilievile, kunatajwa kuwapo kwa kazi ya kuhamisha hospitali nne, kutoka majengo ya zamani kwa ujenzi katika maeneo mapya, ikigusa hospitali rufani za mikoa: Shinyanga, Singida, Mara na Ruvuma.

Eneo la nne linagusa ukarabati na ujenzi wa majengo mapya ya huduma za afya katika hospitali za rufani na mikoa; Ligula (Mtwara), Sekou Toure (Mwanza), Maweni (Kigoma), Sumbawanga (Rukwa) na Kitete (Tabora). Mwisho inatajwa ni Serikali ya Awamu ya Sita, inavyojenga zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri katika maeneo mbalimbali nchini.

> "Kinachotumika sasa ni awamu ya kwanza ya ujenzi wa hospitali hii (mjini Mpanda), lakini kuna awamu ya pili na awamu ya tatu kama inavyoonyeshwa kwenye ramani. Fedha za ujenzi wa awamu ya pili tayari zimeshafika.

**SIKU ALIPOKUWA KATAVI**

Ilikuwa Julai 14, mwaka huu, Rais Dk. Samia alitembelea Hospitali ya Rufani Mkoa Katavi, kujionea hali ya utoaji huduma na mwendelezo wa miradi ya ujenzi ambako kuna ujenzi.

Hapo akasema, serikali inaendeleza jitihada za kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, kwa kuboresha miundombinu ya kutoa huduma, kuanzia ngazi ya msingi, ili kuimarisha huduma za afya nchini.

Rais Dk. Samia akasema, serikali tayari ilishapeleka fedha za ujenzi wa awamu ya pili ya hospitali hiyo, huku katika kipindi hiki miezi mitatu iliyopita, kulitarajiwa kuongezwa vifaa vya huduma za kibingwa.

"Hizi ni jitihada za serikali kusogeza huduma za afya karibu sana na wananchi, ambapo ndani ya mkoa huu wa Katavi tumefanya kazi ya kuongeza vituo vya afya, hospitali za wilaya, kata hadi kule chini kwenye zahanati.

"Kwa hiyo lengo ni kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Hospitali kama hizi tulizoea kuzisikia huko Dar es Salaam, Mwanza na Arusha, lakini hospitali hii ipo Katavi.

"Nimekwenda kuangalia wodi ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati nimeona huduma iliyopo pale, ni sawa na huduma iliyopo Dar es Salaam, wodi ya watoto ambao hawakutimiza miezi tisa, mashine za kisasa na wataalamu wapo," akasisitiza Rais.

Lingine lake la nyongeza, ni serikali itaendelea kuimarisha hospitali hiyo kwa ujenzi wa Awamu ya Pili na Tatu, kwa ujenzi wa majengo mengine ya kutoa huduma.

"Kinachotumika sasa ni awamu ya kwanza ya ujenzi wa hospitali hii (mjini Mpanda), lakini kuna awamu ya pili na awamu ya tatu kama inavyoonyeshwa kwenye ramani. Fedha za ujenzi wa awamu ya pili tayari zimeshafika.

"Kwa hiyo, hospitali hii itaendeleza ujenzi kujenga majengo mawili zaidi ya kutoa huduma na tutaendeleza ikamilike kama ilivyo kusudiwa kwenye ramani," anaeleza Rais.

Pia, akatumia fursa hiyo kuwasihi wananchi wa mkoa wa Katavi na Tanzania kwa ujumla kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. "Niwaombe sana watakapokuja Mfuko wa Bima kwa Afya, kila mwananchi anunue bima yake na familia yake mara moja kwa mwaka unatibiwa na familia yako mwaka mzima."




Hospitali ya Rufani Lindi (MITWERO), Rais Dk. Samia Suluhu Hassan aliweka jiwe la msingi, Septemba mwaka jana. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

AFYA

# TAMASHA UTAMADUNI NA SAIKOLOJIA YA KABURI LA CHIFU LENYE MAAJABU

## •Akichinjwa kuku, damu yake inatoweka
## •Nyoka anayeonekana baada kila miaka 5
## •Alizikwa amekaa, akiwa na wenye uhai 2

**Na Elizabeth Zaya**

KUELEKEA Tamasha la Kitaifa la Utamaduni, linaloanza kati ya Septemba 20 hadi 23 mwaka huu, kuna makubwa ya kisakolojia katika maisha ya umma huo, hasa wakazi wa kijiji cha Mbingamharule wilayani Songea, mkoa wa Ruvuma.

Hapo hija inateka saikolojia na fikra zao, wakiwa na mitazamo chanya nayo, ikiwamo kinachotambuliwa kama "kaburi lenye maajabu la kiongozi kimila, Chifu Ngosi Mharule bin Zulu Gama."

Agnes Ngonyani, Msimamizi wa Kaburi hilo la kihistoria, ambalo sasa limejengwa umbo la duara kwenye eneo la ekari nne, ni moja ya vitu sasa vinapata hadhi ya kitalii, kijijini hapo.

Chifu Mharule, alitokea nchini Afrika Kusini na kwenda kutawala katika kabila hilo la Wangoni kuanzia mwaka 1847 hadi 1889 alipofariki na kuzikwa kijijini hapo.

Historia inaonyesha kuwa baada ya kufariki Chifu Mharule, alizikwa kwa kufuata desturi na mila za kichifu za kabila la Wangoni toka Afrika Kusini na wakati anazikwa, walichukuliwa watu wengine wawili hai na kuzikwa naye kwenye kaburi moja.

"Chifu Mharule baada ya kufariki mwaka 1889, alizikwa kwa taratibu za jadi ya machifu wa Afrika Kusini, kaburi lake lilikuwa la mviringo, sanda yake ilikuwa ya ngozi.

"Alikalishwa, kwenye kiti cha ngozi na walichukuliwa na watu wengine wawili wakiwa hai, ambao walizikwa pamoja naye kwenye kaburi moja wakiwa wamesimama mbele na nyuma ya mwili wa Chifu," anasimulia Ngonyani.

Anasema kwa historia ya mila na desturi ya Kingoni, taratibu za kijadi za wakati huo zilitaka mfalme au chifu anapofariki, lazima azikwe na watu wawili wakiwa hai na kwamba hiyo ilikuwa ni amri ya serikali ya jadi na hapakuwapo anayepinga.

Kwa mujibu wa Mzee Ngonyani, wengi waliozikwa na Mfalme, ni wale waliozoeana na kufanya kazi kwa karibu.

Mbali na shughuli za utalii, kaburi hilo limekuwa likitumiwa na wananchi kwenda kuhiji kila mwaka na hata ndugu wa Chifu Mharule kutoka Afrika Kusini, huafika kufanya matambiko kwenye kaburi hilo.

"Mwaka 2019 ukoo wa Chifu Mharule kutoka Afrika Kusini ulifika kushuhudia kusimikwa kwa Chifu Nkosi Imanuel Zulu Gama wa Tano, ambaye ndiye Chifu wa Wangoni kwa sasa. Kwa hiyo yeyote anayependa kwenda kutembelea kaburi hilo.



Kinamama wakiomba dua mbele ya kaburi la Chifu Mharule, kwa mila za Kingoni. Picha nyingine, ni mwonekano wa kaburi hilo, lenye umri zaidi ya karne na robo na limetengwa eneo la ekari nne. **PICHA: MTANDAO**



### VYA KUSHANGAZA

"Kuna taratibu zake za kimila, ambazo zinatakiwa kufuatwa ambazo ni kubeba mahindi na ulezi ambao unatengenezwa na bibi katika kijiji hicho.

"Baada ya kufika eneo la kaburi, anatangulia mhusika ambaye anawasiliana na Chifu kwa lugha ya jadi, ndipo waliofika kutambika wanaitwa na kupiga magoti juu ya kaburi na kuomboleza kwa sala za jadi.

"Baada ya maombi kuku au mbuzi wanachinjwa juu ya kaburi la Chifu Mharule, lakini jambo la kushangaza mbuzi huyo anapochinjwa hapigi kelele na baada ya kuchinjwa mmoja wa watambikaji anamwaga unga wote juu ya kaburi," anasimulia Ngonyani.

Anataja lingine analoliita la kushangaza, mtu anapoenda hapo siku inayofuata kwenye kaburi, haoni damu wala unga, ikiwa ishara wanayoamini "kukubaliwa shida zote' ambazo mtambikaji alikwenda nazo kuomba kwenye kaburi hilo.

Agness, ambaye amepewa kazi ya kusimamia kaburi hilo kwa sasa, anasema wamekuwa wakipokea wageni wengi wanaotembelea kaburi hilo na kwamba wapo ambao wanatoka mpaka nchi za Ulaya, Marekani na Afrika ambao nao huenda kuomba kutatuliwa shida zao mbalimbali, kuhiji na kufanya matambiko.

Agness anasema, maajabu mengine yaliyopo katika kaburi hilo ni pamoja na kuwapo kwa nyoka ambaye huonekana baada ya miaka mitano au kumi ambaye hata hivyo anapojitokeza kwa kipindi hicho ni watu watu ambao hubahatika kumuona.

"Huyu nyoka haonekani mara kwa mara, isipokuwa baada ya miaka mitano au kumi tena akijitokeza, watu wachache sana ndio hubahatika kumuona na akionekana huwa anaenda bondeni kunywa maji," anasema Agness.

Anasimulia kwamba, eneo hilo la kaburi linaheshimika na hakuna mtu mwenye uthubutu wa kufanya uharibifu wowote.

"Kwa mfano, kwenye kaburi hilo la Chifu Mharule, kuna mtu aliwahi kwenda akaezua paa lakini hakuchukua hata mwezi mmoja alifariki, kwa hiyo tunaamini kwamba sababu hiyo ndio ilisababisha kifo chake," anasema Agnes.

Anataka kwamba eneo hilo la kaburi la Chifu Mharule lenye heka nane linahitaji kuendelezwa na kulindwa, ili maajabu yaliyopo hapo yaendelee kuvutia watalii.

"Eneo lenye nafasi kama hili na lenye historia kubwa linahitaji kulindwa na kuendelezwa ili yale yaliyopo hapa yasipotee, kwa hiyo tunakaribisha wawekezaji, waje wawekeze na kutuinulia mila na desturi zetu zilizoasisiwa na wazee wetu," anasema Agnes.

Septemba 20 mpaka 23 mwaka huu linafanyika Tamasha la Kitaifa la Utamaduni na miongoni mwa vivutio vya utalii wa kitamaduni vinavyobeba idadi kubwa ya watalii hususani katika kipindi hiki linapofanyika tamasha hilo ni wengi wao kushuhudia kaburi hilo la maajabu.

Rais Samia Suluhu Hassan, ndiye anatarajiwa kufunga tamasha hilo siku ya kilele chake Septemba 23 mwaka huu, hivyo mwangalizi wa kaburi la Chifu Mharule anasema ujio wake mkoani Ruvuma huenda ukaongeza idadi kubwa ya watalii wanaotembelea eneo hilo la kaburi.

"Ujio wa Tamasha la Kitaifa la Utamaduni kwenye mkoa wetu, kwetu ni fursa ya kutuongezea watalii kwenye vivutio vyetu, na hata ujio wa kiongozi mkubwa kama Rais unasaidia kutuletea watu wengine wengi, kwa hiyo tunawaalika waje kutembelea na kujionea maajabu yaliyopo kwenye kaburi hili la Chifu Mharule,"anasema Agnes.

"Tunanaamini kwamba Rais Samia (Samia Suluhu Hassan naye akija kufanya utalii hapa kwetu, ataguswa na vivutio hivi vya utalii wa kiutamaduni na kuviendeleza," anasema.

Hadi sasa mkoa wa Ruvuma, umo katika maendeleo yenye vivutio vingi vya utamaduni na ndipo hata serikali ikaelekeza Tamasha la Kitaifa la Utamaduni, kuenzi mambo yanayofanana na hayo.

## MAPINDUZI MAJI TANGA KUTOKA HATARI UKAME, HADI MWELEKEO KUJITOSHELEZA

Inatoka Uk. 11

85.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (UWASA), Mhandisi Geofrey Hilly, anamuunga mkono Mkuu wa Mkoa akisema kukamilika kwa mradi huo wa kimkakati, upatikanaji wa maji safi na salama katika Jiji la Tanga kufikia upeo wa juu zaidi ya makadirio yaliyoko.

Mhandisi Hilly, anasema imeingia mkataba na kampuni inayosimamia ujenzi wa Bomba la Mafuta (EACOP), katika kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wilaya za Muheza na Tanga.

Mhandisi Hilly, anasema kuwa fedha hizo zitatekeleza miradi miwili ya maji, matokeo yake ni kunufaisha wananchi 30,000 kwa huduma hiyo.

Msimamizi wa Ujenzi wa EACOP Kituo cha Tanga, Jerome Betat, anasema mradi huo ni sehemu ya kurudishia faida jamii jirani na mradi.

Mnamo Machi mwaka 2021, Dk. Samia alipokuwa Makamu wa Rais, aliweka jiwe la msingi la Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mji wa Muheza wenye thamani ya Sh. bilioni 6.1, kukabili changamoto ya upatikanaji maji uliokuwa katika mji wa Muheza na vijiji jirani.

Hivi karibuni, Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango, amezindua Uuzaji Hati Fungani ya Kijani ya (Tanga UWASA) yenye thamani Sh. bilioni 53.12, akisifu kitendo chake cha kutafuta uwezeshaji wa kifedha mbadala, unafaa kuigwa na taasisi zote nchini.

Ni kauli inayorejea alichotamka Rais Dk. Samia, kwa kuisifu mamlaka hiyo kwa ubunifu, ikiendesha shughuli zake katika namna ya ubunifu.

Ugeni wa Dk. Mpango katika hatifungani, ulitanguliwa na uwekaji jiwe la msingi la Mradi wa Kuboresha Hali ya Upatikanaji wa Maji jijini Tanga na Wilaya ya Mkinga, wenye thamani Sh. bilioni 53.12 akisema kitendo cha mamlaka hiyo kuamua kutafuta uwezeshaji mbadala ya fedha ni kitendo cha maendeleo.



Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Maji na Mazingira, wakikagua Kituo cha Kusafishia Maji cha Mowe katika kijiji cha Pande, nje kidogo ya Jiji la Tanga. **PICHA: CHEJI BAKARI**

AFYA

# Vijue virusi vinavyolinda mwili wa binadamu, vinakwepana na bakteria

**Na Mwandishi Wetu**

KITAALAMU mwilini, kuna kinachoitwa 'microbiome' - makundi ya bakteria na aina nyingine ndogo za vidudu, ambavyo huishi katika tumbo la mwanadamu. Imebainika kuwa bakteria hao wana virusi ambavyo vipo ndani na nje yao na vina faida kwa mwanadamu.

Pia, vipo vinavyojulikana kama 'bacteriophages' au kwa jina jingine 'phages,' ndani ya mfumo wa usagaji chakula wa binadamu.

Breck Duerkop, Mtaalamu wa Bakteria katika ngazi ya chuo kikuu, anasema watafiti wanaamini ikiwa madaktari wanaweza kuvipata virusi sahihi, vinaweza kuboresha afya ya binadamu.

"Kutakuwa na virusi vizuri na virusi vibaya," anasema Paul Bollyky, daktari wa magonjwa ya kuambukiza na mtafiti katika Taasisi ya Stanford Medicine.


Lakini hadi sasa, bado haijabainika ni virusi vingapi hukaa kwenye tumbo. Vilevile, kuna virusi vingine bado havijatambulika. Sehemu kubwa ya utafiti wa sasa wa virusi ni kutambua virusi hivi na bakteria wanaoishi nao.

"Aina zao ni za kushangaza," anasema Colin Hill, mwanabiolojia katika Chuo Kikuu cha Cork, huko Ireland. Wanasayansi hupata virusi kutoka katika sampuli za kinyesi cha binadamu.

Virusi hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Pia, anasema hubadilika kulingana na umri, jinsia, chakula na mtindo wa maisha, kama Hill na wafanyakazi wenzake walivyoeleza katika utafiti wao wa mwaka 2023.

Ingawa virusi huambukiza bakteria na wakati mwingine huwaua, uhusiano wa bakteria na virusi bado ni ngumu kuuelewa.

"Tulikuwa tukifikiri kwamba virusi na bakteria wanapigana," anasema Hill, aliongeza "lakini sasa tunajua kwamba wanaishi pamoja na ni washirika."



Kirusi mlinzi wa binadamu. **PICHA: MTANDAO.**

**MANUFAA YA VIRUSI**

Inaelezwa, kila mtu ana virusi vya kipekee vinavyoingiliana kila mara na bakteria wa utumbo na vinaweza kunufaisha kwa bakteria kwa kuleta jeni mpya.

Wakati chembe za virusi zinapokusanyika ndani ya bakteria, kirusi hicho kinaweza kuingiza jeni za bakteria kwenye ganda lake la protini pamoja na jeni zake mwenyewe.

"Baadaye, huzifanya jeni hizo kuwa jeni mpya, ni jeni zilizohamishwa kwa bahati mbaya na zinaweza kusaidia," anasema Duerkop.

Virusi huwaweka bakteria katika hali nzuri, anasema mtaaalamu Hill. Bakteria wanaweza kuwa na kinga hadi 12. Kinga tofauti zinatajwa kuwa na faida tofauti; kuepuka mfumo wa kinga mwili au kukaa kona tofauti ya mfumo wa utumbo.

Hill anasema bakteria ni lazima kila wakati wabadilishe kinga zao, ili kukwepa virusi vinavyotambua kinga moja tu. Matokeo yake, wanakuwa na uwezo wa kushughulikia changamoto mpya.

Virusi pia huzuia idadi ya bakteria wasizidi kupita kiasi. Wanautaja utumbo kuwa ni mfumo wa kiikolojia kama misitu na virusi ni wawindaji wa bakteria, kama mbwa mwitu na wawindaji wengine.

Utumbo unahitaji virusi kama vile msitu unavyohitaji mbwa mwitu. Wakati uhusiano wao unapobadilika, ugonjwa unaweza kutokea.

Watafiti wameona mabadiliko ya virusi kwa watu wenye ugonjwa wa tumbo (IBS), kama kuharisha na saratani ya utumbo mkubwa, mfumo wa ikolojia wa mtu aliye na shida hizo mara nyingi huwa tofauti.

Hill anasema wanasayansi wanatafuta virusi vinavyoweza kutumiwa kimatibabu dhidi ya bakteria wanaosababisha vidonda vya tumbo.

"Nadhani, tunapaswa kushukuru kwa matrilioni ya virusi vinavyosimamia mfumo wa ikolojia ya utumbo. Bila wao, aina fulani ya bakteria zinaweza kutawala haraka - na uwezekano wa kushindwa kusaga baadhi ya vyakula na kukabiliwa na gesi, hutokea," anasema Hill.

- ***Makala hii ni kwa mujibu wa BBC.***



## HABARI DODOMA

# UVCCM yalaani vijana kutumika kuvuruga amani

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

BARAZA Kuu la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) limetoa maazimio matatu ikiwamo kulaani vyama vya siasa na asasi za kiraia wanaowatumia vibaya vijana kuharibu amani.

Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Mohamed Ali Mohamed (Kawaida), aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa baada ya kikao cha baraza kilichoketi Septemba 17, mwaka huu.

Alisema kikao hiko kimetoka na maazimio hayo na wajumbe walilaani vikali wanaowatumia vibaya vijana katika kuharibu na kubeza amani iliyopo, umoja na mshikamano wa taifa na kamwe UVCCM haitavumilia matendo hayo.

Aidha, alisema baraza limetoa wito kwa vijana wenye sifa, kujitokeza kwa wingi kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kujiandikisha katika daftari la makazi, kugombea na kupiga kura.

Katika hatua nyingine, alisema baraza limepongeza serikali zote mbili zinazoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa namna zinavyoendelea kuwatumikia wananchi kwa vitendo kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 hadi 2025.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, George Simbachawene (kushoto), akizungumza na viongozi mbalimbali, wakati wa ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa chumba cha maabara ya Shule ya Sekondari Mtera Dam, Kata ya Mtera, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: UTUMISHI**

# Mbunge ataka makandarasi wababaishaji kunyimwa miradi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MBUNGE wa Singida Kaskazini, Ramadhan Ighondo, ametaka makandarasi wababaishaji wasipewe zabuni ya mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Ngimu kilichoko Halmashauri ya Wilaya ya Singida kitakachogharimu Sh.milioni 687.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Ngimu alipofanya ziara iliyolenga kusikiliza kero na kuzipatia ufumbuzi.

Akiwa katika kikao hicho, Ighonda alisema tayari fedha za ujenzi wa kituo hicho zimeshaingizwa kwenye akaunti na kilichobaki ni kumpata mkandarasi wa kuanza ujenzi.

"Makandarasi wababaishaji wasipewe zabuni wala nafasi katika ujenzi wa kituo hiki, kwa sababu watakwamisha ujenzi kwa kuwaibia wananchi na kurudisha nyuma juhudi za Rais Samia za za kuwaletea wananchi maendeleo," alisema.

Mbunge huyo alisema baadhi ya makandarasi wanaopewa zabuni za ujenzi wa miradi mbalimbali wamekuwa wababaishaji na kukwamisha miradi jambo ambalo linazorotesha jitihada za serikali za kuwaletea maendeleo wananchi.

Ighondo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia fedha nyingi za mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Ngimu na kuwataka wananchi kujitolea nguvu zao. Alisema: "Ni miaka 14 tangu niingie madarakani nimepambana vya kutosha kila nilipopata fursa nilikisemea kituo hiki sasa kitajengwa kuanzia msingi mpaka kikamilika. Rais Samia ametupatia fedha nyingi jimboni kwenye miradi mingi sana na sisi hatuna deni naye kwa sababu tunamwahidi kumpa mitano tena aendelee kuwaletea wananchi maendeleo."

Pamoja na mambo mengine, mbunge huyo aliwaomba wananchi kutoa taarifa kwa mtu yeyote yule atakayehujumu fedha za mradi huo, ili kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Pamoja na hayo, alitoa wito kwa jamii kusimama imara kulinda na kutunza miundombinu yote katika miradi iliyojengwa katika kata hiyo ikiwamo maji, umeme, barabara, zahanati na vyumba vya madarasa.

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Dk. Grace Ntogwisangu, alisema kuwa ujenzi wa Kituo cha Afya Ngimu utaanza Oktoba mwaka huu na kuwataka wananchi kuchangia nguvu kazi ya asilimia ili ujenzi huo ukamilike haraka.

# 'Shule za wanafunzi wenye uhitaji tumieni msaada vizuri'

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

MKURUGENZI wa shirika lisilo la kiserikali la Kisedet, Anderson Ndonu, ameziasa shule zenye wanafunzi wenye ulemavu zinazopatiwa misaada ya vifaa mbalimbali vya kielimu kuhakikisha vinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alitoa wito huo jana mkoani hapa wakati akizungumza na wananchi baada ya kukabidhi msaada wa kompyuta 10 zenye gharama ya Sh. milioni tano kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Viziwi ya Kigwe.

Alisema lengo la watoaji wa vifaa hivyo vya elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu ni kuona vinatumika kutimiza ndoto yao kitaaluma.

Aidha, aliwaomba wahisani na serikali kuendelea kuwakumbuka wanafunzi wa shule hiyo, kuwaondolea kero zinazowakabili ili wafanye vizuri kwenye masomo yao.

Kadhalika, alisema kuwa wadau hao wa elimu wakijitoa kwa kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu watawapunguzia changamoto wanazokabilia nazo kwa upande wa elimu, malazi, chakula na afya.

Alisema kuwa msaada huo wa komputa zilizotolewa umelenga kuwawezesha wanafunzi hao kujifunza mbinu mbalimbali za kielimu, ili wafanye vizuri kwenye ufaulu kama ilivyo kwa shule zinginezo ambazo zina vifaa kama hivyo.

Alisema kuwa wanafunzi hao wenye ulemavu wakisaidiwa mahitaji taifa litaweza kuwapata viongozi mbalimbali ambao watakaoliongoza kwa malengo ya kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Alisema: "Shirika hilo la Kisedeti lisilo la kiserikali tumekuwa na utamaduni wa kuwakumbuka wanafunzi kwa kuwapatia misaada mbalimbali, hivyo niwaombe wahisani pamoja na serikali kuwasaidia pale inapohitajika kufanya hivyo".

Naye Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Thadei Mhwagile, alisema kuwa wanafunzi hao wana changamoto nyingi zinazohitaji kutatuliwa kwa kusaidiwa na wahisani mbalimbali.

Hivyo aliwaomba wadau na taasisi mbalimbali zenye uwezo kufika na kutoa misaada kwa wanafunzi kwa sababu bado wanauhitaji mkubwa wa vifaa kwa kufanyia kazi pamoja na kusomea.

"Tunawaomba wadau kuunga mkono juhudi za shirika hili la Kisedet ambalo limekuwa wakiwakumbuka mara kwa mara wanafunzi hawa wenye uhitaji kwa kuwapatia vifaa mbalimbali," alisema.

Nao baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo waliomba wahisani wakiwamo serikali, mashirika, taasisi za kidini na watu binafsi kuwakumbuka kwa kuwapatia misaada mbalimbali ikiwamo vifaa vya elimu ili kufanya vizuri kwenye masomo yao kitaaluma.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, mmoja wa wanafunzi hao, Giolana Selestino alisema kuwa msaada ulitolewa kwa upande wao utawawezesha kuwapunguzia vikwazo vinavyowakabili ili wafanye vizuri kielimu.





# Ukataji miti ovyo wamkera waziri, atoa onyo

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WANANCHI wilayani Makete mkoani Njombe wameonywa kuacha tabia ya kukata miti ovyo ili kuondokana na mabadiliko ya tabia za nchi.

Wito huo ulitolewa juzi na Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana wakati akizungumza na wananchi kwenye mkutano uliofanyika Kata ya Isapilano wilayani humo.

"Tusikate miti ovyo, tukikata miti tutakuwa jangwa na tukiwa jangwa tutakosa mvua na tukikosa mvua tutakosa chakula," alisema Dk. Chana.

Dk. Chana alisema kila eneo utakalopita katika Wilaya ya Makete linavutia kwa kupandwa miti kila mahali na hivyo kuwataka kuendeleza utamaduni huo bila ya kuacha kwa sababu soko la bidhaa za mbao pia lipo.

"Kupitia taasisi yetu ya TFS tutaendelea kutoa mbegu za miti ya kutosha, tunazo shule zetu za sekondari, tunazo shule zetu za msingi na maeneo mbalimbali, hivyo ni wajibu wetu kuwa na maeneo ambayo yatapandwa miti," alisema Dk. Chana. Hata hivyo, Waziri Dk. Chana alisema kwamba pamoja na zoezi la utunzaji mazingira lakini kuna tatizo la uchomaji moto misitu ambalo limekuwa likiharibu miti na miche.

**"Kupitia taasisi yetu ya TFS tutaendelea kutoa mbegu za miti ya kutosha, tunazo shule zetu za sekondari, tunazo shule zetu za msingi na maeneo mbalimbali,..**

"Kwa hiyo suala la moto Serikali ya Kijiji tumeweka utaratibu mtu akitaka kusafisha shamba kwa kuchoma moto unapaswa kufanya nini, usiwe peke yako lazima uwe na watu, lazima uombe kibali ili ule moto usihame kwa hiyo niwaombe sana ndugu zangu tutunze misitu, tutunze mazingira," alisema Dk. Chana.

Baadhi ya wananchi wilayani Makete, akiwamo Alfayo Sanga alisema bado kuna matukio mengi ya misitu ya kupandwa kuungua moto, sababu kubwa ikiwa ni kuandaa mashamba.

"Ukitembea huko tayari watu wameanza kuandaa mashamba, wanachoma tu moto ambao unahama na kuingia kwenye mashamba ya watu wengine ambao wanafanya kilimo biashara cha miti, wanalia kwa sababu wanaishia kupata hasara tu," alisema Sanga.

Hivyo, aliiomba serikali kuingilia kati tatizo la uchomaji moto na sio kuliacha ngazi za vijiji pekee, badala yake washirikiane kwa kutamka adhabu kali ambayo itamfanya mtu asirudie.



Ofisa Uwekezaji na Msimamizi wa Dawati la Mashariki ya Kati wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Juma Nzima (kushoto), akifafanua jambo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya GSG Energies, Ismael Elazhari (kulia), wakati wa kuwapokea wageni wa Kampuni ya Al-Sobat Group, kutoka Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam juzi, wanaokuja nchini kwa ajili ya kuwekeza katika sekta mbalimbali kwa kushirikiana na GSG Energies. Wa pili kushoto ni Mwenyekiti wa Makampuni ya Al-Sobat Group, Hisham Hassan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Raia wa kigeni mbaroni tuhuma wizi wa fedha

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linawashikilia raia wa kigeni wawili kwa tuhuma za kujihusisha na matukio ya wizi wa fedha na mali za wananchi ikiwamo kufungua milango ya magari na kuiba. Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Ally Kitumbi, alieleza hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa na kuwataja watuhumiwa hao ni Fikiri Omary (40) na Humphrey Nyairo (22).

Alisema watuhumiwa hao walikuwa na kawaida ya kwenda kwenye benki wakiwa na gari na kuwavizia wanaotoka, kisha kuwafuatilia ili kwenda kuwaibia fedha. Alisema kwamba watuhumiwa hao walikuwa na funguo bandia za magari wanapoifuatilia gari, endapo mhusika akipaki sehemu wao wanafungua na kuchukua mali zilizopo ikiwemo fedha, kisha wanafunga milango ya gari kwa kutumia fungua bandia na kuondoka.

"Siku hiyo wakati wanakamatwa kuna mtu alikuwa ametoka benki pale Makambako akaingia kwenye gari wakaanza kumfuatilia sasa wananchi pale wakatia mashaka wakampigia simu na kumweleza kuwa kuna watu wapo nyuma wanakufuatilia chukua tahadhari," alisema Kamanda Kitumbi.

Alisema baada ya kupewa taarifa hiyo ndipo mfanyabiashara huyo akatoa taarifa kituo cha polisi na askari wakaanza kuwafuatilia watuhumiwa hao na kuwakamata.

Aidha, alisema watuhumiwa hao walikuwa wanatumia gari ambalo lilikuwa na namba bandia za usajili ambazo ni T 802 DUH wakati namba sahihi za usajili za gari hiyo ni T330 DFP.

Alisema upelelezi wa shauri hilo umekamilika tayari na watuhumiwa hao wamefikishwa mahakamani tangu Septemba nne mwaka huu kujibu mashtaka yanayowakabili.

# Zao la parachichi lazidi kuchanua Mafinga

**Na Renatha Msungu,** MUFINDI

ZAO la parachichi wilayani Mafinga mkoani Iringa, limetajwa kustawi kwa kasi baada ya wataalamu wa kilimo kutoka Shirika la Maendeleo la Rural Development Organisation (RDO) kuhamasisha kilimo cha kitaalamu.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa RDO, Fidelis Filipatali, wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea shamba la parachichi lililoko eneo la Mdabula Halmashauri ya Mji wa Mufindi wilayani hapa.

Filipatali alisema siri kubwa ya mafanikio katika zao hilo ni kutokana na wataalam wa kilimo ambao hutoa elimu katika kilimo hicho cha biashara.

Alisema RDO wamekuwa wakifuata kanuni na taratibu za kilimo wanazoelekezwa na wataalam wa kilimo wa shirika hilo pamoja na wale wa serikali.

"Kilimo mkoani hapa kinastawi sana na hii inatokana na wakulima kulima kilimo cha kisasa kwa kufuata maelekezo kutoka kwa wataalam wa kilimo," alisema Filipatali.

Alisema wanafanya hivyo kutokana na kuhitaji kufanya kilimo chenye tija ambacho kitawanufaisha wakulima ikiwemo kuwainua kiuchumi.

Aidha alisema hivi sasa serikali iko mstari wa mbele kuhakikisha inatafuta masoko ya mazao mbalimbali ndani na nje ya nchi sambamba na kuwahimiza wakulima kulima zao hilo kwa wingi.

"Sio kwenye zao la parachichi pekee, hata kwenye kilimo cha nyanya RDO tunalima kitalaam ndio maana tuvuna kwa wingi mazao ya nyanya," alisema.

Alisema mazao hayo ni ya muhimu kwa jamii na yana soko kwa sababu yanahitajika na wananchi kila iitwapo leo kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Filipatali alisema shirika limejiwekea mikakati ya kuhakikisha wanaendelea kuwa mstari wa mbele kuendesha kilimo cha kisasa na kuacha na zana ya kilimo cha mazoea ambacho hakina faida.

Alisema: "Wakulima wanapaswa kulima kisasa ili waweze kuvuna parachichi nyingi pamoja na nyanya ambazo zitawainua kiuchumi wao na familia zao".

## UVCCM: Hatutawavumilia wanaowatumia vijana vibaya

**Na Gwamaka Alipipi**

BARAZA Kuu la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), limesema halitavumilia vitendo vya mtu, vyama vya siasa, asasi za kiraia za ndani na nje ya nchi, jumuiya za kimataifa watakaowatumia vibaya vijana katika kuharibu na kubeza amani, umoja na mshikamano wa taifa.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mwenyekiti wa UVCCM-Taifa, Mohammed Ali Kawaida jijini Dodoma katika kikao cha kawaida cha baraza hilo ambacho pamoja na mambo mengine kilijadili masuala mbalimbali na kutoa maazimio.

Alisema miongoni mwa maazimio hayo ni pamoja na kutoa wito kwa vijana wote wenye sifa, kujitokeza kwa wingi kwenye mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kujiandikisha katika Daftari la Mpigakura pamoja na lile la makazi.

Kawaida alisema UVCCM itawaunga mkono vijana hao wakaojitokeza katika nafasi mbalimbali za uchaguzi.

Aidha, alisema baraza hilo kwa kauli moja wamezipongeza serikali zote mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) inavyoongozwa na Dk. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), chini ya Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa namna zinavyoendelea kuwatumikia wananchi.

Alisema viongozi hao wamefanikiwa kuongoza wananchi vizuri kwa vitendo kupitia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

# Wananchi wakoshwa huduma bure matibabu macho

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wa Kisiwa cha Pemba wamesema kuletewa huduma za matibabu ya macho bure kutawapunguzia gharama, kutokana na wengi wao kuwa na kipato kidogo.

Walisema hayo jana wakati wakizungumza na Nipashe kwenye utoaji wa huduma za macho zinazotolewa na Taasisi ya Bilali Mission Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Tigo-Zantel.

Mmoja wa wakazi hao, Khamis Mohamed Ussi mkazi wa Uweleni, alisema matibabu hayo yamewafikia muda mwafaka kwa sababu jamii inakabiliwa na tatizo la ugonjwa wa macho na wengi wao hawana uwezo wa kufuata matibabu hayo maeneo ya mbali.

Maryam Issa Haji na Mboje Hamad wakazi wa Mwambe walisema ujio wa madaktari bingwa wa magonjwa ya macho kutawarahisishia kupata tiba sahihi na kuondokana na athari za magonjwa ya macho.

Alisema: "Wengi wetu tunapoanza kusumbuliwa na tatizo la macho, tunatumia dawa za asili kumbe wakati mwingine ndiyo tunaongeza tatizo bila ya kujua, hivyo ni vyema nawasihi wananchi wenzangu kufika kwa wataalamu wa afya kupata tiba sahihi".

Latifa Saleh Ali mwanafunzi wa Shule ya Uweleni, alizitaka taasisi zinazotoa msaada wa kimatibabu ya afya kufika shuleni kutoa huduma za afya kwa wanafunzi kwa sababu wapo wanasumbuliwa na magonjwa mbalimbali ikiwemo tatizo la macho ambayo matibabu yake yanahitaji fedha nyingi.

**Mkurugenzi wa Tasisi ya ya Bilali Muslim Mission of Tanzania, Kharu Nbanu Alibhai, alisema wanatarajia kuwafikia wananchi zaidi ya 3,000 katika kuwapatia huduma za**

Mkurugenzi wa Tasisi ya ya Bilali Muslim Mission of Tanzania, Kharu Nbanu Alibhai, alisema wanatarajia kuwafikia wananchi zaidi ya 3,000 katika kuwapatia huduma za matibabu ya macho.

Alisema Sh. milioni 70 zitatumika katika zoezi hilo la siku tatu la utoaji wa matibabu bure lililoanza juzi katika Shule ya Sekondari Uweleni mkoani Pemba.

Alisema matibabu hayo ni bure na wananchi watapatiwa miwani, dawa na kufanyiwa upasuaji kwa wale watakaogunduliwa na tatizo.

Meneja wa Kanda wa Taasisi ya Tigo- Zantel Pemba, Said Massoud Ali, alisema lengo la matibabu hayo ni kuwasaidia wananchi ambao wako mbali na vituo vya kutolea huduma hizo kwa kupatiwa huduma ya upimaji wa macho na kupata ushauri wa kitaalamu.

Alisema kambi kama hizo zinafanyika sehemu mbalimbali na wanaamini taifa lenye wananchi wenye afya ni lenye nguvu na linaloweza kupata maendeleo ya haraka.

Sheha wa Uweleni, Abdalla Omar Mjawiri, alisema hatua hiyo ya utoaji wa matiabu ni ya kiungwana na taasisi hizo zimeonesha mapenzi kwa wananchi katika kuwapatia matibabu bure hatua ambayo inaungwa mkono na serikali.



Mwakilishi wa Viti Maalum Wanawake Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mwanajuma Kassim (kulia), akijadiliana jambo na Mwakilishi wa Viti Maalum Wanawake mkoa huo, Chumu Khamis Kombo, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mama, baba lishe kunufaika mpango matumizi nishati safi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMA na baba lishe zaidi ya 10,000 nchini wanatarajia kunufaika na kampeni ya matumizi ya nishati safi ya kupikia lenye lengo la kupambana na mabadiliko ya tabia nchi, kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan.

Kampeni hiyo kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO) na kampuni ya ndani Moto Safi, inatarajia kusambaza vifaa vya kupikia vinavyotumia ethanol kwa wauzaji wa chakula nchini kote, ikiunga mkono juhudi za serikali kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo, Mkurugenzi wa kampuni za Said Salim Bakhresa, Hussein Sufiani alisema majiko 500 ya kupikia ethanol yatasambazwa katika Jiji la Dar es Salaam, huku mipango ikitarajiwa kufika katika mikoa yote nchini.

"Takriban asilimia 80 ya kaya za Tanzania zinategemea mkaa na kuni kwa ajili ya kupikia, ambayo ni sawa na kaya milioni nane. Kutegemea hivi kumepoteza zaidi ya asilimia 25 ya eneo la misitu ya Tanzania," alisema.

Alisisitiza kuwa ethanol ni moja ya vyanzo vya nishati mbadala vinavyopatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu Tanzania.

Mei mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua mkakati wa kitaifa wa nishati ya kupikia safi wa miaka 10 ukiwa na bajeti ya Dola za Marekani bilioni 1.8 (trilioni 4/-), akitoa maagizo ya kuwezesha utekelezaji wake na kushughulikia mabadiliko ya tabianchi.

Wakati wa uzinduzi huo, Rais Samia alionyesha wasiwasi kuhusu hatari zinazotokana na mbinu zisizo salama za kupikia, kama vile kuni na mkaa.

Hivyo, aliiomba mkakati huo kuunganishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050 na kupendekeza kuanzishwa kwa mfuko maalum wa kukusanya rasilimali kwa ajili ya upatikanaji wa nishati ya kupikia safi.

Naye, Mwakilishi wa UNIDO, Victor Hakim, aliwahimiza wahusika wa mpango huu kupanua wigo wake ili kuhakikisha kwamba sehemu kubwa ya wananchi wanaweza kunufaika.

# Afya ya mama na mtoto yabeba Tanzania kimataifa

**Na Romana Mallya**

ENEO la afya ya mama na mtoto ni moja ya kigezo kilichobeba Tanzania kufanyika kwa mkutano wa Merck Foundation Africa Asia Luminary 2024, ambalo mdhamini wake ni Rais Samia Suluhu Hassan.

Merck Foundation ambayo ni shirika la misaada la Merck KGaA Ujerumani, itafanya Toleo la 11 la Luminary lake la kila mwaka liitwalo "Merck Foundation Africa Asia Luminary" na kufanyika kwa siku mbili kuanzia Oktoba 29, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo jana jijini huku akieleza kuwa hicho ndicho kigezo kikubwa kilichobeba Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo mkubwa utakaohudhuriwa pia na wake wa marais 13 wa Afrika.

"Kuhusu hali ya mama na mtoto Tanzania ni kigezo kilichosababisha pia nchi yetu kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huu na maombi yakaletwa na Rais Samia na kuyaridhia.

Dk. Gwajima alisema ipo kasi ya ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na hospitali na vifaa vikifungwa kuwahudumia watanzania na watumishi wakiajiriwa.

"Tunafanya vizuri eneo la afya ya mama na mtoto tukiangalia miaka mitano nyuma tulikuwa na vifo vingi 556 kwa vizazi hai 100,000, lakini tumefanya vizuri mpaka vikafika vifo 104 kwa vizazi hai 100,000 na sasa hadi kufikia mwaka 2030 tunatakiwa kufikia viwango vya Malengo ya Milenia vya vifo 72 kwa vizazi 100,000.

"Tuna furaha kuandaa luminary hili lenye hadhi kubwa nchini Tanzania ambalo linawakutanisha wake wa marais wa Afrika, mawaziri, watunga sera, wataalamu, watoa huduma za afya na waandishi wa habari kutoka nchi zaidi ya 70," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Merck Foundation na Mwenyekiti wa Merck Foundation Africa Asia Luminary, Seneta, Dk. Rasha Kelej, alisema, "Tunafurahi kutangaza Toleo la 11 la Luminary letu la kila mwaka kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania, litakalozinduliwa rasmi na Rais Samia."

Kadhalika, aliwakaribisha wageni, watoa mada mbalimbali pamoja na wake wa marais wa Afrika na mabalozi wa Kampeni ya 'More Than a Mother'.

"Ninasubiri kwa hamu kushiriki uzoefu wetu na kujadili athari za programu zetu katika kuboresha huduma za wagonjwa na kuongeza uelewa kuhusu masuala mengi nyeti na muhimu ya kijamii na afya.

"Luminary hili litafunguliwa rasmi na Rais Samia, pamoja na Prof. Dk. Frank Stangenberg-Haverkamp, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Merck Foundation na kuongozwa naye (Seneta Kelej), huku wake wa marais wa Afrika kutoka nchi zaidi ya 15 wakiwa wageni rasmi na wasemaji wakuu," alisema. Prof. Dk. Frank Stangenberg-Haverkamp, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Merck Foundation, alisema Merck Foundation ina dhamira ya kuboresha afya na ustawi kwa kuimarisha uwezo wa huduma za afya na kutoa ufumbuzi wa afya bora na sawa katika Afrika, Asia na kwingineko.

Kulingana na taarifa yao kwa vyombo vya habari, luminary hiyo litafanyika kwa njia mseto, likijumuisha ushiriki wa ana kwa ana na mtandaoni kwa zaidi ya watoa huduma za afya 6,000, watunga sera, wataalamu, watafiti, na wawakilishi wa vyombo vya habari vya afya kutoka nchi zaidi ya 70 barani Afrika, Asia, na kwingineko. Kati yao, washiriki 500 watahudhuria ana kwa ana.

"Nchi zinazoshiriki katika Toleo la 11 la Merck Foundation Africa Asia Luminary ni pamoja na: Angola, Bangladesh, Benin, Botswana, Burkina Faso, Burundi, Kameruni, Canada, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Kambodia, Chad, Côte d'Ivoire na Jamhuri ya Kongo.

"Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Ethiopia, Ufaransa, Gabon, Ujerumani, Ghana, Guinea-Bissau, Guinea-Conakry, India, Indonesia, Kenya na Lesotho.

"Liberia, Malawi, Malaysia, Mali, Mauritania, Mauritius, Mexico, Msumbiji, Myanmar, Namibia, Nepal, Niger, Nigeria, Peru, Ufilipino, Urusi, Rwanda na Senegal," ilisema.

# Jaji Mkuu ajivunia mfumo wa Tanzil kudhibiti rushwa ndogo

**Na Grace Gurisha**



JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amesema kupandisha hukumu za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani katika Mfumo wa Mahakama unaochapisha uamuzi na sheria mbalimbali (Tanzil), kumeondoa tatizo la rushwa ndogo kwa wananchi kupata nakala za hukumu.

Amesema lengo la kupandisha katika tovuti hiyo ni kuweka kila kitu kwa uwazi, hukumu ikitolewa tu inatakiwa kupanda muda huohuo ili wananchi wasome.

Prof. Juma alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa siku mbili kuhusu upatikanaji taarifa za uamuzi wa mahakama hizo na sheria mbalimbali zinazopatikana kidigiti.

Alisema mfumo huo wa Tanzil umewawezesha wananchi wengi zaidi kupata uamuzi badala ya kusubiri kwa njia ya karatasi wakati wanaanza mchakato wa maboresho ya eneo ambalo waliliona lina changamoto -- upatikanaji nakala za hukumu.

" Wakati huo ilikuwa ukitaka kupata nakala ya hukumu hasa kesi za madai, ulikuwa unatakiwa uhesabu kurasa, kila ukurasa ni Sh. 2,000 unalipa, kwa mwananchi wa kawaida kuweza kukusanya fedha kulipa kurasa hata 10 wengi ilikuwa ni shida.

"Vilevile, kwa mwananchi wa kawaida kuweza kusoma zile hukumu ilikuwa ni vigumu na kabla ya maboresho tuliona kwamba upatikanaji nakala za hukumu kwa urahisi ilikuwa ni eneo ambalo Tume ya Warioba ya Rushwa iliona ndiyo mwanya wa hizi rushwa ndogo," alisema Prof. Juma.

Jaji Mkuu alibainisha kuwa rushwa hiyo ilikuwa inatokea pale mtu anapokwenda kuomba nakala ya hukumu, anazungushwa hata kulazimika anatoa fedha kidogo kupata anachokitaka.

"Sasa sisi tukaona kwamba tukiwa na uwazi upatikanaji nakala za hukumu tutaweza kabisa kuondoa tatizo la rushwa, hukumu inaposomwa inatakiwa ipandishwe wakati huohuo katika mifumo ya Tanzil.

"Safari yetu mara ya kwanza tulivyokwenda kujifunza, tulituma watumishi wetu Afrika Kusini, Namibia na Nigerian, lengo wakati huo lilikuwa kutaarisha majuzuu ya sheria, lakini walipotembelea kule wakakuta wenzetu wanapandisha uamuzi katika mifumo ya tovuti ndiyo wakaja na hayo mawazo," alisema.

Jaji Mkuu alisema kuwa kuanzia mwaka 2018, wakaanza kupandisha taarifa hizo, ambapo kwa sasa kuna nakala zaidi ya 1,000 za uamuzi wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani zimeshapandishwa kuanzia mwaka huo hadi sasa.

Alisema kuwa badaye wenzao wa Afrika Lii na Shirika la GIZ la Ujerumani wakaona wawasaidie kwenda kufukua uamuzi wa zamani kuanzia 2018 kurudi nyuma ili upandishwe na huo mchakato unaendelea.

"Hii itasaidia wananchi wa kawaida kuweza kufanya utafiti wao wenyewe kama kuna suala anaweza kuangalia 'nikipeleka suala hili mahakamani uwezekano wa kushinda unakuaje, kwa hiyo lengo hasa kuwawezesha wananchi wawe na uwezo kuendesha kesi zao," alisema.

Jaji wa Mahakama ya Rufani, Dk. Paul Kihwelo alisema mfumo wa Tanzil unarahisisha upatikanaji wa taarifa za kidigiti za uamuzi wa mahakama na sheria mbalimbali pamoja na kanuni za mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi wa Sheria wa Taifa.

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAID ALLY KULUNGE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha Sita chenye Index No. **S5472-0565** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SAVANA PLAINS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021, Cheti hiki kimepotea mkoani Geita. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/41586/2024**

## KUMBUKIZI YA KIFO
### CHA MWALIMU OTILIA BARNABAS HAULE



"Tunashukuru kwa jina la bwana wetu, amani iwe nanyi. Leo ni mwaka mmoja tangu tumempoteza mpendwa wetu mama, mke, na dada **OTILIA BARNABAS HAULE,** hadi leo haijakuwa rahisi bila yeye, angalau sasa tunajua anapumzika kwa amani na tunaamini roho yake ipo mahali pazuri, kusema hivyo tunamshukuru Mungu kwa muda wote tuliokuwa naye, kwetu ilikuwa ni Baraka na kwa hilo tunamshukuru Mungu milele. Kwa sasa hayo ndiyo yote tunayopenda kusema hadi tutakapo kutana tena, mpendwa wetu Otilia, Mama, Mke, na Dada, unakumbukwa na Mama, Mume wako, Watoto wako, Wadogo zako, Wajomba zako, Mama zako wadogo, Mashemeji zako, Wafanyakazi/walimu wenzako na majirani zako wa Mazimbu na Kihonda/Yespa na Marafiki uliosoma nao,

**Amina"**
**2 TIMOTHEO 4:7 "Umevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo umeumaliza, imani umeilinda"**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**AKIDA MIKIDADI MOHAMEDI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COASTER** yenye usajili namba **T 892 DDC** na CHASSIS NAMBA: **JT743BB4207001606.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/182214/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo Cha HANETI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 02/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU DENIS M SEMGOMBA WA CHENENE-DODOMA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ANNA DENIS SEMGOMBA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 Mwezi 09 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa,
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isioyohusika

Imetolewa leo Tarehe 17 Mwezi 09 Mwaka 2024

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO HANETI DODOMA

## KUPOTEA KWA VYETI



**KIRISHE JOHNAS MBWAMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P.2517-0967** kilichotolewa na **ALPHA SECONDARY SCHOOL CENTRE** Mwaka 2018. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0359-0736** kilichotolewa na **KIGURUNYEMBE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MOR/MOR/30768/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LAMWAY MKOTYO MOGEN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0922-0128** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MWINYI SECONDARY mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/PWA/MKU/18732/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**LINDA THOBIAS NGENDABANYIKWA**

Anatangaza kupotelewa na kadi za gari zenye namba za usajili **T 347DQV, T 126DRZ, T 930DFB,** Kwa yeyote atakaezione atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MOR/MOR/31553/2024**

# Wamarekani waliohukumiwa kifo DRC wakata rufani

**KINSHASA, DRC**

WAKILI anayesimamia kesi ya raia watatu wa nchini Marekani waliohukumiwa kifo huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kwa tuhuma za kushiriki katika jaribio la mapinduzi ya Richard Bondo amewasilisha rufani ya kupinga hukumu ya kifo iliyotolewa dhidi yao.

Mahakama ya kijeshi nchini DRC siku chache zilizopita ilitoa hukumu ya kifo kwa watu 37, wakiwamo vijana watatu wa Marekani ambao ni Benjamin Zalman Polun, Marcel Malanga na Tyler Thompson, baada ya kuwatia hatiani kwa tuhuma za kushiriki katika jaribio la mapinduzi.

Washtakiwa hao, wengi wao wakiwa ni Wakongomani lakini pia Mwingereza, Mbelgiji na Kanada, walikuwa na siku tano za kukata rufani dhidi ya hukumu hiyo kwa tuhuma zinazojumuisha jaribio la mapinduzi, ugaidi na kujiunga na chama cha uhalifu, na kwamba watu 14 waliachiliwa huru katika kesi hiyo.

"Kongo ni mwanachama wa Mkataba wa Roma, na kwa sababu hiyo kurejeshwa kwa hukumu ya kifo ilikuwa kinyume cha sheria, bunge lilipaswa kuamua juu ya adhabu mbadala, lakini haijafanya hivyo hadi sasa," alisema Wakili Bondo.

Ilielezwa kuwa DRC ilirudisha hukumu ya kifo mapema mwaka huu, na kuondoa usitishaji uliodumu kwa zaidi ya miongo miwili, huku mamlaka ikijitahidi kuzuia ghasia na mashambulizi ya wanamgambo nchini humo.

Pia ilielezwa kuwa wanaume waliopatikana na hatia katika jaribio la mapinduzi wanaweza kuuawa kwa kupigwa risasi.

Aidha, Jeshi la Kongo lilisema matu mmoja aliyetambulishwa kwa jina moja Malanga aliuawa kwa kupigwa risasi akipinga kukamatwa mara tu baada ya kutiririsha moja kwa moja shambulio hilo kwenye mtandao wake wa kijamii.

Mtoto wa kiume wa Malanga, Marcel Malanga, mwenye umri wa miaka 21, ambaye ni raia wa Marekani, na Wamarekani wengine wawili walihukumiwa katika jaribio hilo la mapinduzi.

***TRT***

# Rais Ufaransa kutimuliwa madarakani

**PARIS, Ufaransa**

OFISI ya Bunge la Ufaransa imeidhinisha utaratibu wa kutimuliwa kwa Rais wa taifa hilo, Emmanuel Macron uliowasilishwa na baadhi ya wabunge wa Chama cha New Popular Front (NPF).

Ilielezwa kuwa wakati Ufaransa inasubiri serikali yake mpya kwa miezi miwili, Chama cha NFP kinabaini kwamba mkuu wa nchi anafanya walichodai kuwa ni (mapinduzi dhidi ya demokrasia). Na kwamba utaratibu huu unaonekana kutokuwa na nafasi ya kufanikiwa.

Pia ilibainishwa kuwa Ofisi ya Bunge ndiyo ilikamilisha mkutano wake na sasa imethibitishwa.

Ilielezwa kuwa azimio lililopendekezwa linalolenga kumtimua madarakani Rais Macron litaendelea na mkondo wake katika Baraza la Bunge. Huku NPF ikiwa na wingi wa kura katika ofisi hiyo, azimio hilo limepitishwa kwa kura 12 dhidi ya 10.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo haijawahi kushuhudiwa nchini humo kwasababu awali hakuna utaratibu wa kumtimua kiongozi wa nchi uliowahi kufika mbali kama wa sasa. Na kwamba miaka 10 iliyopita, pendekezo lililowasilishwa na mrengo wa kulia dhidi ya François Hollande lilikataliwa katika hatua ya ofisi.

Ilibainishwa kuwa hatua hiyo inauwezekano, isifanyike kwasababu njia ya kutekeleza kifungu cha 68 cha katiba imejaa vikwazo karibu visivyoweza kushindwa.

Ilielezwa kuwa theluthi mbili ya wabunge na maseneta watalazimika kupiga kura kuunga mkono azimio hilo mbele ya Mahakama Kuu ya Jamhuri, ambayo inawaleta pamoja wabunge 11 na maseneta 11, kuchukuwa uamuzi.

Hata hivyo, makundi mengi katika Bunge yanapinga suala hilo, ikiwa ni pamoja na ndani ya Chama cha NPF. Pamoja na wasoshalisti waliotangaza kwamba hawatapiga kura kuunga mkono nakala hiyo..

***RFI***



Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, akiwa Elysée. **PICHA: MTANDAO**

# Korea Kaskazini yaendelea kuimarisha silaha za kivita

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

SHIRIKA rasmi la Habari la Korea Kaskazini (KCNA) na gazeti la Rodong Sinmum limetoa picha kadhaa zikimwonyesha kiongozi wa taifa hilo, Kim Jong Un akitembelea kile ambacho vyombo hivyo vimesema ni kituo cha kurutubisha uranium.

Ilielezwa kuwa ilikuwa mara ya kwanza kwa Korea Kaskazini kufichua kituo cha kurutubisha uranium hadharani.

Katika hotuba ya hivi karibuni ya kuadhimisha miaka 76 toka kuanzishwa kwa serikali yake, Kim alisema Korea Kaskazini, itaongeza maradufu juhudi zake ili kufanya vikosi vyote vya kijeshi vya serikali, pamoja na jeshi la nyuklia, kuwa tayari kikamilifu kwa mapigano.

Wakati huo huo, Korea Kusini na Japan zilisema, Korea Kaskazini ilirusha makombora mengi ya masafa mafupi Jumatano ambayo yalitua baharini katika pwani yake ya mashariki.

Makombora hayo yalirushwa kutoka Kaechon, kaskazini mwa mji mkuu, Pyongyang, majira ya saa 12:50 asubuhi kwa saa za huko na kuruka kuelekea kaskazini mashariki, Mnadhimu wa jeshi la Korea Kusini alisema bila kutaja idadi ya makombora yaliyofyatuliwa.

"Jeshi letu linaendelea kuwa tayari huku likiimarisha ufuatiliaji na umakini kwa majaribio hayo huku tukisambaza habari kwa haraka kwa Marekani na Japan," ilisema taarifa.

Takribani dakika 30 baada ya taarifa ya kwanza ya kombora, idara ya ulinzi wa pwani ya Japan, ilisema Korea Kaskazini ilirusha kombora lingine na kuanguka. Huku Komandi ya Indo-Pacific ya Marekani, ikisema kupitia mtandao wa X, inafahamu majaribio hayo na imeshauriana na Seoul na Tokyo.

***VOA***

# Israel yashutumiwa kuishambulia Lebanon

**BEIRUT, Lebanon**

WANAMGAMBO wa Hezbollah wameitupia lawama Israel kwa madai ya kufanya mashambulizi nchini Lebanon na kusababisha vifo vya watu tisa, majeruhi 2,800 huku wengine 200 wakiwa katika hali ya mahututi.

Ilielezwa jana kuwa shambulio hilo lilisababisha mamia ya vifaa vya mawasiliano vilivyokuwa vikitumiwa na wanachama wa kundi la wanamgambo wa Hezbollah na raia wa kawaida kulilipuka katika maeneo mbalimbali kote nchini Lebanon.

Kundi la wanamgambo wa Hezbollah liliapa kulipa kisasi dhidi ya shambulio hilo la Jumanne likisisitiza kuwa Israel imehusika, na kwamba litaiadhibu.

Ilielezwa kuwa mapema jana, vifaa hivyo ambavyo ofisa mmoja wa Hezbollah alisema kuwa ni vipya, vilianza kupata moto na kisha kuripuka.

Jeshi la Israel halijazungumza lolote kuhusu shambulio hilo. Na kwamba awali ilitangaza kuwa inataka kutanua vita vyake kwenye Ukanda wa Gaza hadi Lebanon.

Kiongozi wa Hezbollah, Hassan Nasrallah awali aliwatahadharisha wanachama wa kundi hilo kutotumia simu za viganjani akisema kuwa zinaweza kutumiwa na Israel kufuatilia nyendo zao.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Iran, IRNA, balozi wa nchi hiyo huko Lebanon, Mojtaba Amani, alijeruhiwa na moja ya kifaa kilicholipuka na alikuwa akipatiwa matibabu.

Iran yenyewe iliishutumu Israel kwa shambulio hilo ililoliita kuwa ni mauaji ya halaiki. Huku Waziri wa Mambo ya Kigeni Nasser Kanan, katika taarifa yake akilaani kitendo hicho alichokitaja kuwa cha kigaidi.

Hata hivyo, Russia kupitia wizara yake ya mambo ya kigeni, nayo pia ililaani shambulio hilo iliyoliita baya kabisa.

Vile vile, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Anthoniy Blinken ambaye yuko mjini Cairo ili kuokoa juhudi za kupata makubaliano ya kusitisha vita katika Ukanda wa Gaza. Makubaliano hayo yanazidi kukabiliwa na ugumu hasa baada ya shambulio la vifaa vya mawasiliano lililowalenga wanamgambo wa Hezbollah.

***DW***

# Malindi yataka 'Top 4' Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BENCHI la ufundi la klabu ya Malindi FC, limesema moja ya malengo yao makubwa msimu huu ni kuhakikisha wanamaliza kwenye nafasi nne za juu ,Top 4' katika msimamo wa Ligi Kuu ya Zanzibar inayoshirikisha timu 16.

Malindi kwa sasa inaongoza Ligi kwa kuwa na pointi sita baada ya kupata ushindi kwenye michezo yake yote miwili iliyocheza mpaka sasa.

Akizungumza na Nipashe, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Suleiman Mohamed ,Mo', alisema suala la ubingwa kwao ni kipaumbele cha mwisho, kwa sasa lengo lao ni kumaliza kwenye nafasi hizo.

„Kama itatokea tumechukua ubingwa itakuwa vizuri zaidi, lakini kwa sasa kwanza lengo letu ni kuwa kwenye nafasi nne za juu, ligi ni ngumu lakini tutapambana katika michezo yetu yote ili kutimiza lengo letu," alisema Mo.

Aidha, alisema wanachoangalia zaidi ni kuhakikisha timu hiyo mpaka inakamilisha mzunguko wa kwanza kabla ya kuingia mzunguko wa pili wa lala salama wanaendelea kusalia katika nafasi nne za juu.

Alisema matokeo mazuri waliyoyapata yametokana na juhudi kubwa zinazofanywa na wachezaji wenyewe uwanjani hasa kwa kufuata maelekezo ya benchi lao la ufundi.

"Tunapambana kwanza tuwe katika nafasi hizi za juu muda wote wa msimu huu wa Ligi, na tutafanikiwa hili iwapo wachezaji watazidisha kujituma katika michezo yetu yote," alisema.

Aidha alisema kuwa licha ya mafanikio ya michezo miwili lakini bado anahitaji kulifanyia kazi eneo lake la ulinzi ili kutoruhusu wapinzani wao kupenya kirahisi.

# MGUTO AWATOA HOFU MASHABIKI COASTAL

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kushuhudia Coastal Union ikipata kipigo cha pili kwenye michezo yao mitatu ya Ligi Kuu, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Steven Mguto, amesema timu hiyo itarudi kwenye uwezo wake na kuanza kupata ushindi.

Akizungumza baada ya mchezo wao dhidi ya Namungo FC uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex wanaoutumia kama uwanja wao wa nyumbani, Mguto, alisema matokeo waliyoyapata ya kufungwa mabao 2-0 yamewaumiza lakini wanaendelea kujipanga kwa ajili ya mchezo ijayo.

"Si matokeo mazuri, lakini ndivyo mpira ulivyo, mpira siku zote una matokeo ya aina tatu, kufungwa, kufunga au kutoka sare, bado tuna nafasi ya kufanya vizuri, ndio kwanza tumecheza michezo mitatu tu," alisema Mguto.

Aidha, alisema uongozi wa klabu hiyo unaendelea na mchakato wa kutafuta kocha mpya wa timu hiyo kwa ajili ya kuchukua nafasi ya aliyekuwa kocha wao, David Ouma ambaye walimtimua kutokana na kufanya vibaya kwa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Tupo kwenye mchakato wa kutafuta kocha mpya, ligi bado sana, kuna michezo mingi mbele yetu, naamini tutakaa sawa na kuanza kufanya vizuri zaidi, ukiangalia kwa sasa tumecheza michezo mitatu tu, kuna michezo mingi mbele," alisema Mguto.

Coastal kabla ya mchezo wa juzi, pia ilitoka kupoteza mbele ya Mashujaa FC kabla ya kulazimishwa sare mbele ya KMC.

Mchezo ujao Wagosi hao wa Kaya wataumana na Azam FC ukiwa mchezo wao wa nne tangu kuanza kwa msimu huu wa Ligi Kuu, mchezo huo utachezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex Jumapili ijayo.




Mchezaji wa Timu ya Soka ya Bulls, Sabillah Sidique, akijaribu kuwatoka wachezaji wa Timu ya Soka ya Mtoni Sabasaba Sports Center, walipokutana kwenye mchezo wa kirafiki katika Uwanja wa Gymkhana, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kiungo Singida avunja rekodi bao la mapema Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Singida Black Stars, Emmanuel Keyekeh, amevunja rekodi ya kufunga bao la mapema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, mchezaji huyo raia wa Ghana alifunga bao pekee dhidi ya Pamba Jiji sekunde ya 20 ya mchezo, akivunja rekodi iliyowekwa na straika wa Dodoma Jiji, Paul Peter, ambaye Alhamisi iliyopita alifunga bao sekunde ya 39.

Peter alifunga bao hilo Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Dodoma Jiji ikiichapa Namungo bao 1-0, Keyekeh naye juzi alipachika bao pekee lililoipa ushindi Singida Black Stars ikiwa ugenini.

Lilikuwa bao la pili kwa mchezaji huyo kwenye Ligi Kuu ambaye amesajiliwa msimu huu kutoka Samartex FC inayocheza Ligi Kuu nchini Ghana.

Agosti 17, mwaka huu, alifunga bao moja Uwanja wa Sokoine Mbeya wakati timu yake ikiifunga KenGold mabao 3-1.

Ulikuwa ni ushindi wa asilimia 100 kwa Singida, ikiwa imeshinda mechi zote nne walizocheza mpaka sasa kwenye Ligi Kuu.

Ilianza kwa kuifunga KenGold mabao 3-1, Kagera Sugar bao 1-0, KMC mabao 2-1, kabla ya juzi kupata tena ushindi, ukiwa ni wa tatu ikiwa ugenini.

Kocha Mkuu wa Singida, Patrick Aussems, alisema timu yake imecheza vyema hasa kipindi cha kwanza, ingawa kipindi cha pili haikuwa kama alivyotarajia kutokana na mabadiliko aliyoyafanya.

"Tulifanya mabadiliko kipindi cha pili kitu ambacho kilifanya tushindwe kucheza vizuri," alisema.

Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Goran Copunovic, amewapongeza Singida akisema walistahili kushinda huku akilia na uchanga wa wachezaji wake.

"Hatukuwa na kitu chochote ambacho kingeweza kuwazuia, tumejitahidi sana lakini ubora wao umeamua," alisema kocha huyo raia wa Serbia.

Huo ulikuwa mchezao wa kwanza Pamba Jiji kupoteza baada ya kucheza mechi nne ikiwa nafasi ya 10, lakini haijafunga bao lolote ikiwa na pointi tatu baada ya kutoka suluhu kwenye michezo mitatu.

## ZISIKUPITE

### MADRID YASAKA NYOTA

REAL Madrid inalenga kuwanunua kiungo wa kati wa Manchester City na Hispania, Rodri, beki wa pembeni wa Liverpool mwenye miaka 25, Trent Alexander-Arnold na beki wa Arsenal, William Saliba (23), au beki wa kati wa Tottenham na Argentina Cristian Romero (26). ***(Independent)***

### ADEYEMI AIVUTIA UNITED

KLABU ya Manchester United inavutiwa na mshambuliaji wa Borussia Dortmund Mjerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 22, lakini wanaweza kukabiliana na ushindani kutoka kwa Newcastle na Liverpool. ***(TeamTalks)***

### GOMES ATAKIWA EPL

KLABU ya Newcastle United ni miongoni mwa timu za Ligi Kuu England maarufu EPL zinazomtaka kiungo wa kati wa Lille ya Uingereza, Angel Gomes mwenye miaka 24, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Football Insider)***

### GORETZKA ATAKIWA ENGLAND

WEST Ham na Manchester United zinamtaka kiungo wa kati wa Ujerumani, Leon Goretzka mwenye umri wa miaka 29, ambaye hana furaha baada ya kupoteza nafasi yake Bayern Munich. ***(Sun)***

### PICKFORD MUHIMU EVERTON

EVERTON inamwona mlinda mlango wa England, Jordan Pickford, kama mmoja wa wachezaji wake muhimu na hawana mpango wa kumbadilisha. ***(Teamtalk)***

### MARTIAL KUTUA ATHENS

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 28, anakaribia kuhamia AEK Athens kama mchezaji huru baada ya kuondoka Manchester United msimu uliopita. ***(Fabrizio Romano)***

### SANE AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL na Newcastle United huenda zikamnunua winga wa Ujerumani, Leroy Sanem mwenye umri wa miaka 28, ambaye anaripotiwa kutokuwa na furaha katika klabu ya Bayern Munich. ***(Caught Offside)***

### SOLET AGOMBEWA EPL

KLABU za Aston Villa, Nottingham Forest, Wolves na West Ham ni miongoni mwa timu zinazomvutia mlinzi wa Ufaransa, Oumar Solet mwenye umri wa miaka 24 wa Red Bull Salzburg. ***(HITC)***

### LIVERPOOL YASAKA MLINZI

LIVERPOOL inataka kiungo mkabaji na beki wa kati wa upande wa kushoto Januari. ***(Football Insider)***

### ARSENAL YAMWINDA DAVID

ARSENAL inamfuatilia mshambuliaji wa Canada, Jonathan David, mwenye umri wa miaka 24, ambaye anaingia mwaka wa mwisho na Lille. ***(Caught Offside)***

### FULHAM, WOLVES VITANI

KLABU za Bournemouth, Fulham na Wolves zinavutiwa na mlinzi wa Cameroon, Joel Matip, mwenye umri wa miaka 33, ambaye bado ni mchezaji huru baada ya kuondoka Liverpool msimu uliopita ***(HITC)***.

## DONDO… A SOKA MAGAZ… A ULAYA



# KANE AIPIKU REKODI YA ROONEY UEFA

●●●Ni ya kupachika mabao katika Ligi ya Mabingwa huku...

**MUNICH, Ujerumani**

HARRY Kane alifunga mara nne na kufikisha mabao 33 kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hadi kupita rekodi ya awali ya magoli 30 iliyowekwa na Wayne Rooney ya kufunga mabao mengi zaidi katika michuano hiyo.

Ilikuwa ni sehemu ya usiku wa rekodi kwa mshambuliaji huyo na Bayern Munich, waliposhinda 9-2 dhidi ya Dinamo Zagreb ya Croatia katika raundi ya kwanza ya michezo katika mtindo mpya wa Ligi ya Mabingwa.

Mabao tisa ya Bayern pia yalikuwa mengi zaidi kuwahi kufungwa katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa kwa timu moja, na Kane alikuwa na rekodi nyingine ya Ulaya kwa sifa yake na mabao yake matatu akifunga kwa mkwaju wa penalti.

„Mchezo wa kushangaza,“ alisema Kane akimwambia mtangazaji wa DAZN.

"Kufunga mabao hayo yote mwisho wake ulikuwa usiku mzuri.

"Kusema kweli, baada ya bao la pili sikujua la kufanya na lile la tatu."

Kane alitangulia kufunga kwa mkwaju wa penalti na kuwafanya Bayern waongoze na kusawazisha alama za Rooney kwa Mwingereza.

Alifunga bao lake la 31 kwa mpira wa kurejea uliompita Rooney na kuongeza mengine mawili kwa mkwaju wa penalti na kumfanya afikishe mabao 12 katika Ligi ya Mabingwa tangu ahamie Bayern mwaka mmoja uliopita.


„Ana ari na kwangu kama kocha ni rahisi zaidi kwa sababu ukiwa na mchezaji wa kiwango cha juu kama yeye mwenyewe amehamasishwa sana kurahisisha mambo,“ alisema kocha wa Bayern, Vincent Kompany baada ya mechi.

"Yeye ni kiongozi, nahodha wa timu ya taifa. Wachezaji kama yeye, wanajua wanapaswa kuinuka wakati huu na ndivyo anafanya."

Raphael Guerreiro, Michael Olise, Leroy Sane na Leon Goretzka pia walifunga mabao kwa Bayern.

Kane sasa ana mabao 53 katika mechi 50 za michuano yote tangu ahamie Bayern na amefunga mabao tisa katika michezo yake mitatu iliyopita kwa klabu na taifa, yakiwamo mawili ya England dhidi ya Finland katika mchezo wake wa 100 wa kimataifa na hat trick ya Jumamosi kwa Bayern dhidi ya Holstein. Kiel kwenye Bundesliga.

# GUARDIOLA AELEZEA SABABU HAALAND KUPACHIKA MABAO



**MANCHESTER,** ENGLAND

PEP Guardiola anaamini Erling Haaland ameshinda matatizo yake ya kimwili na amerejea katika ufungaji wake bora zaidi.

Baada ya msimu wa kwanza uliovunja rekodi nchini England, idadi ya mabao ya Haaland ilishuka kidogo mnamo 2023/24, na kufunga 38 katika michezo 45.

Hata hivyo, msimu huu anatesa safu ya ulinzi kote England kwa mara nyingine tena hadi kufikia idadi ya mabao tisa katika mechi zake nne za kwanza, ikijumuisha hat-trick mbili, na Guardiola anaamini usawa wa Haaland unatokana na kiwango chake kipya.

"Tofauti na msimu uliopita, anahisi mwili wake uko," alisema Guardiola.

"Alikuja kutoka Dortmund akiwa na matatizo mengi, matatizo ya misuli katika mwezi wa kwanza, na alijitahidi kidogo. Kufikia sasa msimu huu anahisi 'Mimi ni safi, niko vizuri hapa na hakuna matatizo.'

"Sitarajii kufunga mabao mawili au matatu katika kila mchezo, si tatizo kwa sababu najua ubora upo, lakini tofauti na msimu uliopita anajisikia vizuri, hana matatizo, wachezaji wanapokuwa na hisia hizo wanaweza kufanya vizuri zaidi."

Haaland aliwasili kutoka Borussia Dortmund akiwa na sifa ya mmoja wa washambuliaji wakuu wa Ulaya, lakini Guardiola alikiri hata alishangaa kuona mchezaji huyo wa miaka 24 akifikisha mabao hayo.

"Kidogo kwa mshangao," alisema Guardiola.

"Unajua nini, nilicheza miaka 11 nikiwa Barcelona na nilifunga mabao 11. Jamaa huyu alifunga mabao tisa katika mechi nne. Anaweza kunifikia katika mchezo mmoja zaidi! Kwa hiyo amenishangaa!"

# Ten Hag sasa ni kicheko tu

**MANCHESTER,** ENGLAND

ERIK ten Hag alipongeza "usiku mzuri" baada ya Manchester United kuishinda Barnsley mabao 7-0 kwenye Kombe la Carabao.

Marcus Rashford, Alejandro Garnacho na Christian Eriksen wote walifunga mara mbili huku Antony akifunga kwa penalti wakati Ten Hag akiandikisha ushindi mkubwa zaidi katika utawala wake.



Ulikuwa pia ushindi mkubwa zaidi wa United tangu kuifunga Southampton 9-0 Februari mwaka, 2021 chini ya bosi wa zamani Ole Gunnar Solskjaer.

"Sio kwangu bali kwa timu hii ni usiku mzuri kabisa," alisema Ten Hag.

"Nadhani tunaweza kufanya kila kitu tulichopanga kufanya; jinsi tunavyoshinda, raundi inayofuata, kufunga mabao mazuri, kuwaburudisha mashabiki, tulifanyia kazi mtindo wetu wa mchezo kwa hivyo tuna furaha."

Ten Hag aliweza kuzungusha kikosi chake dhidi ya timu hiyo ya League One na kufanya mabadiliko manane kutoka kwa timu iliyoilaza Southampton 3-0 Jumamosi.

Rashford alikuwa mmoja wa wachezaji watatu walioanza na ilikuwa ni mara ya kwanza kwa mshambuliaji huyo wa England kufunga zaidi ya moja katika mchezo mmoja tangu kufunga mabao mawili katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Leicester Februari mwaka, 2023.

"Ninajua tangu msimu wangu wa kwanza hapa kwamba anapofunga ni nzuri kwa timu, ni rahisi zaidi," alisema Ten Hag.

"Unapokuwa na mchezaji katika kikosi chako ambaye ni hakikisho la mabao basi inaweza kuleta mabadiliko. Unaweza kufanya mambo mengi vizuri sana."

United wamefanikiwa kurejea katika kipigo cha mabao 3-0 kutoka kwa Liverpool.

"Sikuwa na huzuni baada ya Liverpool na sasa sisherehekei," alisema Ten Hag.

"Ni mchakato usioisha, najua nataka kwenda wapi, katika mwelekeo gani, najua tuna kasi, nguvu na tumeona hii leo na tuna wachezaji wenye uwezo wa kutawala mpira, lazima tufanye kazi, ngumu zaidi kupata hatua zote za mchezo sawa."

# Martial kujiunga na AEK Athens

**ATHENS,** UGIRIKI

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Anthony Martial anasemekana kukaribia makubaliano ya kujiunga na miamba ya Ugiriki, AEK Athens kwa uhamisho wa bure.

Martial alishindwa kupata klabu mpya wakati wa dirisha la kiangazi licha ya kuondoka United mwishoni mwa Juni baada ya kumalizika kwa mkataba wake.

90min iliripoti mnamo Agosti, mwaka huu wakati Mfaransa huyo alikuwa mvumilivu kuhusiana na mustakabali wake, madai yake ya mshahara yalikuwa yakiziweka kando klabu katika ligi tano bora za Ulaya - ilikuwa ni kwa sababu hii kwamba kurejea katika timu yake ya utotoni ya Lyon hakufanikiwa.

Katika wiki za hivi karibuni, dili na klabu ya Brazil Flamengo lilishindikana, lakini Fabrizio Romano anaripoti Martial 'anakaribia' kuhamia AEK badala yake.

AEK walikuwa na shughuli nyingi wakati wa dirisha la kiangazi, wakiwakaribisha winga wa zamani wa Tottenham Hotspur, Erik Lamela, kiungo wa zamani wa Juventus Roberto Pereyra na kipa wa Brentford Thomas Strakosha katika mji mkuu wa Ugiriki.

Pia walikuwa na matumaini ya kumnunua mshambuliaji wa Chelsea, David Datro Fofana kwa mkopo wa awali na kipengele cha ununuzi cha pauni milioni 20, lakini mazungumzo yalivunjika na mchezaji huyo wa Ivory Coast akaelekea Uturuki katika klabu ya Goztepe.

Ripoti za awali kutoka Ugiriki zilidokeza kuwa AEK walikuwa tayari kumpa Martial mkataba mnono zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Martial alicheza mechi 19 katika mashindano yote katika msimu wake wa mwisho huko United, akifunga mabao mawili pekee.

Katika takriban mwongo mmoja akiwa Old Trafford, alifunga mabao 90 na asisti 47 katika mechi 317.

Sasa akiwa na umri wa miaka 28, Martial atatumaini kuweka nyuma matatizo yake ya jeraha na kuendeleza msururu wa michezo na mabao tena.

# MABAO 39 YAFUNGWA LIGI KUU, MATANO NJE YA BOKSI

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali inayoonyesha bado kuna udhaifu wa wachezaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara kupiga mashuti ya mbali, jumla ya mabao 39 yaliyofungwa msimu huu na nyota 30, ni matano yamefungwa nje ya eneo la hatari.

Kwa mujibu wa dawati la takwimu la Nipashe, mabao 34 yamefungwa ndani ya kiboksi cha hatari.

Wakati mabao matano yakifungwa nje ya boksi, mabao saba yamefungwa kwa kichwa, huku straika wa Singida Black Stars, Elvis Rupia, akiaongoza kwa kufunga magoli mawili kwa njia hiyo.

Waliofunga mabao nje ya boksi mpaka sasa ni Emmanuel Keyekeh wa Singida Black Stars, Velentino Mashaka (Simba), Maxi Nzengeli (Yanga), Redemtus Mussa (KMC) na Dickson Ambundo wa Fountain Gate.

Mbali na straika raia wa Kenya, Rupia kuongozwa kwa kufunga mabao mawili ya vichwa, wengine ni Mohamed Damaro wa Singida Black Stars, Che Fondoh Malone, Mashaka na Edwin Balua kutoka Simba, na Redemtus wa KMC.

Jumla ya penalti sita zimeshatolewa mpaka sasa, nne zikitinga nyavuni na mbili zikiota mbawa.

Takwimu za Ligi Kuu Tanzania Bara zinaonyesha katika michezo 25 iliyochezwa mpaka sasa, mechi 16 zimetoa mshindi na tisa timu zimetoka sare.

Hali inaonyesha timu zimejipanga msimu huu kupata ushindi popote pale, mechi nane zimetoa ushindi nyumbani na idadi hiyo hiyo imetoa washindi walioukuwa ugenini.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena leo kwa mchezo mmoja kati ya Azam FC, itakayokwenda kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam kucheza dhidi ya wenyeji KMC.

Wakati Azam FC ikiwa na pointi mbili tu baada ya kutoa suluhu dhidi ya JKT Tanzania na Pamba Jiji ikiwa nafasi ya 12, KMC ipo nafasi ya saba ikikusanya pointi nne.



Wachezaji wa Timu ya Kambai wakiwa na Koplo, Hans Benny Ngollo (wa pili kulia), tayari kushiriki katika mashindano ya Polisi Jamii CUP yenye lengo la kutoa elimu ya jamii, ulinzi shirikishi na kuhamasisha vijana kujitokeza kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kisangani FC iibuka mabingwa wa michuano hiyo na kupewa zawadi ya mbuzi na mipira miwili. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Zahera: Namungo gari limewaka

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam dhidi ya Coastal Union, Kocha Mkuu wa Namungo, Mwinyi Zahera, amesema tayari wachezaji wake wameshaanza kuyashika vyema mafunzo wanayopatiwa.

Namungo ilipata ushindi wa mabao 2-0, ukiwa ni wa kwanza kwenye ligi, tena ikiwa ugenini, baada ya kupoteza mechi zake zote tatu ilizocheza awali, ikifungwa mabao 2-1 dhidi ya Tabora United, 2-0 dhidi ya Fountain Gate, ikiwa nyumbani, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi na bao 1-0 ikiwa ugenini dhidi ya Dodoma Jiji, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati, mkoani Manyara.

"Tatizo letu kubwa haikuwa kucheza vibaya, ilikuwa pale mbele jinsi ya kumalizia, na hilo ndiyo tumelifanyia kazi na sasa limeanza kutoa matunda. Coastal si timu ya mzaha, ni timu ngumu iliyopata michezo migumu ikiwamo ya kimataifa, Kombe la Shirikisho, kwa hiyo kushinda kwetu mabao 2-0, ni mwanzo mzuri na sasa hata wachezaji wetu kisaikolojia watakuwa vizuri, natumai tutaendelea kufanya vizuri," alisema Zahera.

Coastal inatumia Uwanja wa Azam Complex, kutokana na Uwanja wa CCM Mkwakwani Tanga kuwa katika matengenezo. Yalikuwa ni mabao ya Rith Nkoli dakika ya 37 na Pius Buswita dakika ya 45 yaliyoifanya timu hiyo kupata ushindi na kusogea hadi nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Kipigo hicho kimeifanya Coastal Union kushuka hadi nafasi ya 14 ya msimamo ikiwa na pointi moja tu baada ya kucheza michezo mitatu, haijapata ushindi wowote mpaka sasa, ikitoa sare moja na kupoteza miwili.

## Miguel Gamondi apiga mahesabu

INATOKA UK. 24

kundi rahisi au gumu. Mfano kundi letu msimu uliopita lilikuwa gumu, kulikuwa na CR Beloizdad ya Algeria, Al Ahly ya Misri, hatua ya robo fainali tukakutana na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, kwa maana hiyo kujua utafika wapi inategemea na njia unayopitia," alisema Gamondi.

Kauri hiyo ya Gamondi inaweka wazi matumaini yake makubwa ya timu yake kutinga hatua ya makundi kwenye mchezo wao wa Jumamosi utakaochezwa 2:30 usiku dhidi ya CBE ya Ethiopia, Uwanja wa New Amaan Zanzibar.

Hiyo inachagizwa na mchezo wa kwanza uliochezwa Jumamosi iliyopita, Uwanja wa Abebe Bikila, Addis Ababa, Ethiopia, Yanga ilipopata ushindi wa bao 1-0 lililofungwa na mshambuliaji raia wa Zimbabwe, Prince Dube.

Wakati hayo yakiendelea, Meneja wa timu hiyo, Walter Harrison, ameeleza ni kwa nini mchezo huo wa marudiano umepelekwa Zanzibar badala ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ilivyo kawaida.

Alisema baada ya kufanya tathmini wamegundua kuwa Zanzibar kuna mashabiki wengi wa Yanga ambao nao wanahitaji kushuhudia michezo hiyo ya kimataifa.

"Tumeshacheza sana kwenye uwanja huu, kama utakumbuka mechi yetu ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Azam tulipata ushindi, Zanzibar ni sehemu ya Tanzania na tuna mashabiki wengi sana hakuna mtu mwenye shaka na hilo, tulifanya tathmini ya kina na tukaona ni sehemu sahihi ya kwenda kucheza mchezo wetu wa raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika ambao Mungu akijaalia tutaingia kwenye hatua ya makundi," alisema meneja huyo.

## Fadlu: Kazi bado haijaisha

INATOKA UK. 24

kuhakikisha tunatengeneza nafasi nyingi, hatutahitaji kukaa nyuma, lakini lazima tuwe makini kwenye ulinzi, kazi haijaisha mpaka baada ya dakika 90 za mchezo wetu wa marudiano."

"Sitarajii mchezo mwepesi kwa sababu na wao (Al Ahly Tripoli) watakuja kutafuta ushindi au sare yoyote ya magoli, ni jambo ambalo lazima tuwe makini sana, mashabiki waje kwa wingi kuwatia moyo wachezaji wao," alisema Fadlu.

Kufuatia matokeo ya suluhu ugenini, Simba inahitaji ushindi wowote ili waweze kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo ya pili kwa ukubwa ngazi ya vilabu Afrika. Mchezo huo wa marudiano unatarajiwa kuchezwa Jumapili ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Michezo
Alhamisi Septemba 19, 2024
Nipashe

## Kane aipiku rekodi ya Rooney UEFA

UKURASA 21






Beki wa Singida Black Stars, Edward Manyama (kulia), akiruka juu kupiga mpira kwa kichwa mbele ya mchezaji wa Pamba Jiji FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara juzi, Uwanja wa CCM KIrumba, Mwanza. Singida walishinda bao 1-0. **PICHA: SALEHJEMBE**

# Miguel Gamondi apiga mahesabu makundi CAF

## ●●●Asema kucheza robo fainali itategemea na timu atakazokutana nazo kwenye...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU bado wakiwa hawajatinga hatua ya makundi wakisubiri mchezo wa marudiano hatua ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, ameanza kupigia hesabu hatua ya makundi, akiweka wazi ili kufika hatua ya robo fainali au zaidi itategemea zaidi kundi watakalopangwa.

Gamondi amesema kuna wakati inatokea wanapangiwa timu ngumu na kuwa na kazi kubwa ya kusonga mbele.



Gamondi alisema hawezi kusema wanataka kufika wapi kwenye Ligi ya Mabingwa, badala yake sasa hivi wanaangalia makundi tu mpaka pale yatakapopangwa makundi ndipo watakapojua hilo kutokana na aina ya timu ambazo watakutana nazo.

"Yanga ni klabu ambayo kila msimu inatakiwa iwe kileleni, hivyo kufuzu makundi ni jambo ambalo linaweza kutokea na tuna matumaini sana.

"Baada ya hapo huko mbele tutaona nini kitatokea kwani ni bahati pia kwa upangaji wa makundi, unaweza kupata

INAENDELEA UK. 23

# Fadlu: Kazi bado haijaisha

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Simba, Fadlu Davids, amesema bado hawajamaliza kazi ya kusaka tiketi ya kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika na wanatakiwa kupambana kupata ushindi kwenye mchezo wa marudiano dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya.

Akizungumza muda mfupi baada ya kuwasili nchini wakitokea Libya kwenye mchezo wao wa kwanza ambapo ulimalizika bila kufungana, Fadlu, alisema wamemaliza dakika 45 za kwanza na sasa wanajiandaa kwa dakika nyingine 45.

Alisema kimahesabu ni kama Simba wamepata matokeo mazuri kwenye mchezo huo wa kwanza lakini kwake anaona bado kazi haijaisha na kuna jambo la kufanya kuhakikisha wanapata ushindiutakaowapeleka hatua hiyo ya makundi.



"Tunahitaji ushindi, mipango na mahesabu ya mchezo wa kwanza yameishia Libya, lazima tujiandae na kujipanga vizuri kwa mchezo wa marudiano, kwenye mpira hakuna kitu kinachoshindikana," alisema Fadlu.

Alisema kwenye mchezo huo wa marudiano hawahitaji kukaa nyuma muda wote wa mchezo kwa kuwa kitu pekee wanachokihitaji ni ushindi kwenye mchezo huo.

"Tutaingia na mpango madhubuti wa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >